epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

Ijumaa Novemba 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581847

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Waliokopesha vikundi hewa washikwa pabaya

• **Ni** mikopo ya asilimia 10; mwangwi wa TRAT na TRAB nao... *Endelea ukurasa 2*

## TMA: Mvua itasuasua hadi Februari, baada ya hapo 'masika'

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza kwenye mjadala kuhusu kilimo barani Afrika na nishati safi ya kupikia, katika Mji wa Des Moines, Iowa, Marekani juzi. Rais Samia alishiriki mjadala huo kando ya Mjadala wa Kimataifa wa Norman E. Borlaung, ulioandaliwa na Taasisi ya World Food Foundation. Kushoto ni Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinumwi Adesina. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 22

**KLOPP ATETEA UAMUZI WAKE KUTUA RED BULL**



UKURASA WA 3

**Serikali** yazichambua SU 63 zinazotegemea ruzuku, itoe uamuzi

UKURASA WA 4

**NMB** kuchangia bil. 1/- gharama za matibabu ya moyo watoto JKCI



UKURASA WA 12

GENERALI MUSUGURI

**Alipostaafu** akawa m/kiti wa kijiji wa mfano alikoishi Mwalimu Nyerere




Magari yakipita kwenye maji yaliyojaa katika Barabara ya Biti Titi Mohamed, eneo la Akiba, kutokana na mvua iliyonyesha Dar es Salaam jana asubuhi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



## BoT yatoa tahadhari biashara ya fedha chakavu, za kigeni

UK. 3




Scan hapa kutembelea chanel yetu



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dk. Ladslaus Chang'a, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu mwelekeo wa hali ya mvua ya msimu kuanzia Novemba mwaka huu hadi Aprili 2025. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# TMA yatoa mwelekeo mvua miezi sita

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa mwelekeo wa msimu wa mvua kwa miezi sita, zinazotarajiwa kunyesha kuanzia mwezi huu hadi Mei, mwakani.

Mwelekeo wa mvua za msimu ni katika maeneo ya magharibi mwa nchi, Kanda ya Kati, Nyanda za Juu Kusini Magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa Morogoro, ambayo yanapata msimu mmoja kwa mwaka unaoanza Novemba hadi kati ya Aprili na Mei, mwakani.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alisema jana alipozungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam kuwa mvua inatarajiwa katika kipindi cha nusu ya pili kuanzia Februari hadi Aprili, mwakani ikilinganishwa na nusu ya kwanza ya Novemba, mwaka huu, hadi Januari.

Alisema mvua ya wastani hadi chini ya wastani inatarajiwa katika ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Singida, Dodoma, kaskazini na mashariki mwa mkoa wa Lindi na kaskazini mwa mikoa ya Mbeya na Iringa kuanzia Novemba hadi Aprili, 2025.

Pia alisema mvua ya wastani hadi juu ya wastani inatarajiwa katika mikoa ya Njombe, Ruvuma, Mtwara, kusini magharibi mwa mkoa wa Lindi na kusini mwa mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro.

Dk. Chang`a pia alisema mvua ya wastani hadi chini ya wastani inatarajiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Kanda ya Magharibi, Tabora, Katavi na Kigoma.

"Mvua imeshaanza tangu wiki ya nne ya Oktoba, mwaka huu, katika mkoa wa Kigoma na inatarajiwa kusambaa katika mikoa mingine kwenye wiki ya kwanza ya Novemba na kumalizika wiki ya kwanza ya Mei, mwaka kesho," alisema.

Katika mikoa ya Kati ya Singida na Dodoma, alisema mvua katika maeneo hayo inatarajiwa kuwa ya wastani hadi chini ya wastani na inatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya Novemba na kwisha wiki ya nne ya Aprili na wiki ya kwanza ya Mei, mwaka kesho.

Kwa Nyanda za Juu Kusini Magharibi, alisema mvua ya wastani hadi juu ya wastani inatarajiwa katika mkoa wa Njombe, kusini mwa Mbeya, Iringa na Morogoro wakati zile za wastani hadi chini ya wastani, ikitarajiwa katika mikoa ya Rukwa na Songwe pamoja na kaskazini mwa mikoa ya Mbeya na Iringa katika wiki ya kwanza na ya pili ya Novemba na kuisha wiki ya kwanza ya Mei.

Dk. Chang`a alisema, katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na maeneo ya kusini na magharibi mwa Lindi, mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani wakati katika maeneo ya kaskazini na mashariki mwa Lindi na inatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani.

Alisema mvua hiyo inatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya Novemba kwa mikoa ya Lindi na Mtwara na wiki ya pili na ya tatu ya Desemba kwa Ruvuma huku ikitarajiwa kumalizika wiki ya kwanza ya Mei kwa mikoa ya Ruvuma na Mtwara na wiki ya nne ya Mei kwa Lindi.

"Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vya mvua kubwa zaidi yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani. Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia mvua za msimu wa miezi sita na hali ya mvua katika maeneo makubwa.

"Kwa hiyo viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na kila mwezi," alisema Dk. Chang'a.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
MOSHI

SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA 82 YA 2023

MWANANANCHI ENGINEERING & CONTRACTING COMPANY (MECCO)................................MLETA MAOMBI

VERSUS

KILEMPU KINOKA LAIZER.....................................MJIBU MAOMBI NA.1
STEPHEN KIMAN LAIZER.....................................MJIBU MAOMBI NA.2
THOMAS SINYOCK LAITAYO .....................................MJIBU MAOMBI NA.3
THOMAS SINYOCK LAITAYO .....................................MJIBU MAOMBI NA.3.
THOMAS MORINGE MAKESEN.....................................MJIBU MAOMBI NA.4
JULIUS KESOI LAITAYO.....................................MJIBU MAOMBI NA.5
NOEL MAYASEK LAITAYO.....................................MJIBU MAOMBI NA.6
RICHARD LERUNDA MOLLEL.....................................MJIBU MAOMBI NA.7
NOAH KILEMPU LAIZER.....................................MJIBU MAOMBI NA.8
SINJORE THOMAS LEITAYOK.....................................MJIBU MAOMBI NA.9
AMIRI PANGANI.....................................MJIBU MAOMBI NA.10
MONICA JACKSON.....................................MJIBU MAOMBI NA.11
CHARLES KAAYA.....................................MJIBU MAOMBI NA.12
LAZARO THOMAS .....................................MJIBU MAOMBI NA.13
KUYA KIMANI.....................................MJIBU MAOMBI NA.14
MAGUYA MELEJI.....................................MJIBU MAOMBI NA.15
BARAKA KENYATTA.....................................MJIBU MAOMBI NA.16

**KWA:**
**THOMAS SINYOCK LAITAYO .....................................MJIBU MAOMBI NO.3**
**JULIUS KESOI LAITAYO.....................................MJIBU MAOMBI NA.5**
**NOEL MAYASEK LAITAYO.....................................MJIBU MAOMBI NA.6**
**NOAH KILEMPU LAIZER.....................................MJIBU MAOMBI NA.8**
**SINJORE THOMAS LEITAYOK .....................................MJIBU MAOMBI NA.9**
**AMIRI PANGANI.....................................MJIBU MAOMBI NA.10**
**MONICA JACKSON.....................................MJIBU MAOMBI NA.11**
**CHARLES KAAYA.....................................MJIBU MAOMBI NA.12**
**LAZARO THOMAS .....................................MJIBU MAOMBI NA.13**
**KUYA KIMANI.....................................MJIBU MAOMBI NA.14**
**MAGUYA MELEJI.....................................MJIBU MAOMBI NA.15**
**BARAKA KENYATTA .....................................MJIBU MAOMBI NA.16**

**"POPOTE PALE MLIPO"**

Mnajulishwa kwamba shauri la maombi ya gharama tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa hapa Mahakama ya rufani Kanda ya Moshi tarehe 6/11/2024 saa tatu kamili asubuhi (06:00 mchana.)

Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa nyinyi wenyewe au mwakilishi wenu anayetambulika kisheria, maombi yatasikilizwa bila ya uwepo wenu.

Imetolewa na Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 23/10/2024.

J.J. KAMALA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

# Waliokopesha vikundi hewa washikwa pabaya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kibano kwa waliohusika kutoa kwa vikundi hewa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni alipochangia hoja ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Alisema serikali itachukua hatua dhidi yao ili kukomesha utaratibu wa kuwa na vikundi hewa kwenye mikopo hiyo. Kuhakikisha wanaondokana na changamoto ya fedha ambazo zimekuwa hazirejeshwi zilizokopeshwa kwa vikundi vya ujasiriamali miaka iliyopita, ni kuwapo ufanisi wa marejesho.

"Hadi kufikia Oktoba 30, 2024, jumla ya Sh. bilioni 27 tayari zimekwisharejeshwa na jitihada za kurejesha fedha ambazo zimebakia zinaendelea, hivyo tutahakikisha fedha zote ambazo hazijarejeshwa zinarejeshwa," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema serikali imeshaainisha vikundi vyote vinavyodaiwa na wameshaviweka kwenye kanzidata ili kila kikundi kirejeshe fedha hizo.

Akizungumzia utaratibu mpya wa utoaji mikopo hiyo, Naibu Waziri Dugange alisema serikali imeweka halmashauri 10 za majaribio ya kutoa mikopo hiyo kupitia benki huku halmashauri 174 zitakwenda na utaratibu wa asilimia 10 iliyoboreshwa.

Kuhusu fedha za miradi ya maendeleo, Dk. Dugange alisema halmashauri ambazo hazijapeleka fedha zinazotakiwa kwenye miradi ya maendeleo, wameendelea kuchukua hatua stahiki za kinidhamu ili itekelezwe kadri ya maelekezo na mwongozo wa bajeti.

Katika hatua nyingine, serikali imesema imeimarisha vyombo vinavyohusika na kushughulikia rufani za kodi (TRAT na TRAB) kwa kuteua bodi na kutengeneza timu za wataalamu kwenye mikoa na kwamba kazi hiyo inapaswa kufanywa bila kumwonea mtu wala kupoteza mapato ya serikali.

Akichangia jana bungeni hoja za kamati zinazohusika kuchambua na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema katika utekelezaji majukumu ya TRAB na TRAT, tayari wamekamilisha mapengo yaliyokuwapo kwenye masuala ya uteuzi, yakihusisha kutengeneza bodi na timu za wataalamu katika mikoa ili kufanya kazi ipasavyo.

"Tulirekebisha kanuni kuruhusu wataalamu wale kutumika maeneo tofauti, kazi hizi zinapaswa kufanyika bila kuonea watu wala kupoteza mapato ya serikali, hiki ndicho kinafanyika na kazi inaendelea vizuri.

"Mwezi mmoja uliopita tulikaa na kupokea taarifa hizo na tulikaa pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na tukaona kazi inayoendelea na tunaamini siku si nyingi tutatoa taarifa ya kazi zitakuwa zimekamilika na zile zilizokuwa zinaendelea," alisema.

Kuhusu TRA, alisema kuna maboresho mengi yamefanyika ambapo inajenga mfumo wa forodha na kodi za ndani.

**TIB na TADB**

Alisema serikali imekuwa ikiweka mitaji kuhakikisha kuwa na ufanisi kwenye benki za TIB na TADB.

"TADB imekuwa inapokea mtaji na TIB kazi inayoendelea kwa sasa ni uhakiki wa madeni na taasisi zinazoidai benki hii na kutengeneza mpango ambao itautekeleza wa namna ya kulipa madeni na kuifanya benki kuwa na ukwasi wa kutosha wa kutekeleza majukumu yake," alisema.

**MIRADI YA KIMKAKATI**

Alisema serikali inaendelea kuyapunguza madeni inayodaiwa na wazabuni, makandarasi na kutotengeneza mengine mapya.

"Kazi kubwa imefanyika, tulikuwa tunatenga zaidi ya Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kulipa huduma hizo na mtiririko wa fedha kwenye miradi ya makandarasi wa ndani inatoa kwa wakati ili kuhakikisha hatulimbikizi," alisema.

Ukamilishaji miradi ya kimkakati ambayo imeshafikia hatua ya kukamilishwa, ulisababisha kujibana na kuelekeza nguvu huko na kuathiri mtitiriko kwenye miradi mingine.

"Moja ya miradi ambayo ni fahari ya Watanzania ni Bwawa la Nyerere, tumefinyana na kujifunga mkanda kwa nguvu za watanzania tumeweza kukamilisha na sasa ni asilimia 99 na megawati zimeingia kwenye utekelezaji na sasa serikali inaongeza nguvu kwenye usambazaji ili umeme unafika maeneo yanayohitajika," alisema.

Alitaja mradi mwingine ni Daraja la Magufuli ambalo lipo zaidi ya asilimia 99 ya utekelezaji na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambayo kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma kimeanza kufanya kazi.

"Miradi hii ilichangia kuwapo na mtirirko mdogo wa fedha kwenye miradi mingine, tulikuwa tunabanana ndani ya serikali na kipande kingine kinaendelea na cha Isaka - Mwanza baada ya kupata fedha za mwisho itakamilika na kipande kingine kinaendelea," alisema.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

**HABARI KITAIFA**

## Serikali yazichambua SU 63 zinazotegemea ruzuku

**Na Augusta Njoji,**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema serikali inayachambua mashirika ya umma 63 ambayo yanatengeneza mapato makubwa huku yakiendelea kupokea ruzuku.

Amesema tayari miswada ya sheria ya kuyaunganisha baadhi ya mashirika na taasisi ambazo zinafanana kiutendaji imeandaliwa na itawasilishwa bungeni huku mengine yatafutwa kutokana na utendaji wake kupitwa na wakati.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo jana bungeni alipochangia hoja ya Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) na kufafanua mambo yaliyoibuliwa na wabunge kwenye mashirika hayo.

Katika michango ya wabunge juzi, walionesha kukerwa na baadhi ya mashirika na taasisi za umma kutokuwa na ufanisi katika uendeshaji na kuendelea kutegemea ruzuku, hali inayoisababishia serikali hasara ambapo katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23, utegemezi wa mashirika ya umma umeongezeka kutoka Sh. bilioni 13.2 hadi 17.4 na kushauri serikali iangalie namna ya kuyafunga, kuyafilisi au kuyatafutia ubia na sekta binafsi (PPP).

Waziri Mkumbo alisema serikali inafanya mageuzi makubwa katika uendeshaji mashirika hayo na wanafanyia kazi maelekezo na ushauri wa kamati kuhusu mashirika hayo 63 ambayo yanatengeneza mapato makubwa na bado yanapokea ruzuku ya serikali.

"Hoja ya msingi sana, mashirika haya yanatengeneza mapato makubwa kuliko hata ruzuku wanayopokea, sasa wanapokea ruzuku ya nini? Tunapokea ushauri huu na tutafanya uchambuzi wa kuona namna ya kwenda nayo mbele," alisema.

Alieleza kuwa serikali imefanya uchambuzi wa mashirika hayo na wamebainisha yapo mashirika ya umma ambayo majukumu yao yameshapitwa na wakati ama kwa sababu kwa sasa hayafanywi na serikali au yanaweza kufanywa vizuri zaidi na sekta binafsi na yanayoingiliana na kufanana kimajukumu.

"Lakini pia, yapo mashirika ya umma ambayo serikali imependekeza kwa mujibu wa sheria zao yafutwe na yenyewe mawaziri wa sekta husika watawasilisha hapa, mashirika ya umma ambayo tunadhani yamepitwa na wakati kwa maana ya majukumu yao, yaweze kuchukuliwa hatua kwa kufutwa. "Ni mchakato mgumu kama ambavyo kamati imebainisha na kuona, hakuna mtu ambaye angependa kufutwa au kuunganishwa lakini Mheshimiwa Rais ameshachukua hatua hizo na sisi kama serikali tutakwenda kutekeleza na muda ukifika tutawasilisha miswada husika bungeni kwa ajili ya hatua hizo.

"Yapo mashirika ambayo yanapaswa kufanya biashara lakini hayajaanza kutengeneza faida kwa sababu yapo hatua mbalimbali za kujiendeleza na kujijenga, likiwamo shirika letu la ndege la ATCL," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa mashirika ambayo yanatengeneza hasara kutokana na ufanisi mdogo au kazi ambazo yanazifanya zinapaswa kufanywa vizuri zaidi na sekta binafsi, serikali haitasita kuyafuta.

"Tumepitia maazimio 14 ya Kamati ya PIC na sisi kama serikali tunaahidi kuyapokea na kuyafanyia kazi kwa kuwa ni mazuri yatasaidia kuimarisha mashirika ya umma nchini," alisema.

# Mke wa Rais Malawi afurahia upandikizaji mimba

**Na Joseph Mwendapole**

MKE wa Rais wa Malawi, Monica Chakwera, ameelezea kufurahishwa na huduma za upandikaji mimba zinazotolewa na Kituo cha Kairuki IVF na kusema anatamani kuona huduma kama hizo zinaanza kutolewa nchini mwake.

Aliyasema hayo jana baada ya kutembelea kituo hicho kilichoko Bunju Mianzini, Dar es Salaam na kufahamishwa kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanyika kituoni hapo.

Alisema kituo cha Kairuki IVF kimekuwa msaada kwa wanawake wengi ambao wameshindwa kupata ujauzito kwa njia ya kawaida, hivyo upandikizaji umekuwa ukirudisha furaha kwa wanawake hao. "Nimeambiwa kwamba tangu kianzishwe mwaka 2022 watoto 85 wameshapatikana kwa njia ya upandikizaji mimba. Hii ni taarifa njema kwani watu wengi walihangaika kupata huduma kama hizi Ulaya na mataifa yaliyoendelea lakini sasa zinapatikana kwenye nchi zetu. Hilo ni jambo la fahari sana.

"Sijawahi kusikia kituo kama hiki kwetu Malawi lakini ningependa kuona kinaanzishwa ili kuwapunguzia gharama watu wetu wanaolazimika kusafiri kwenda mataifa yaliyoendelea kutafuta huduma kama hizi," alisema.

Mama Chakwera alisema anatarajia kufanya harambee kwa ajili ya kupata kiasi kikubwa cha fedha zitakazotumika kuwasaidia wanawake wenye shida ya kupata watoto kutumia njia hiyo kumaliza shida zao.

Mkurugenzi wa Kituo cha Kairuki IVF, Dk. Clementina Kairuki, alisema tangu kuanzishwa mwaka 2022, wameshapandikiza wanawake ri na kupata watoto 85 na kwamba mpaka kufikia mwisho wa mwaka huu watakuwa wamefanikiwa kupata watoto 100.

Alisema ndani ya muda mfupi wamefanikiwa kutambuliwa kimataifa kwa kupata ithibati ya ubora (ISO) na kwamba wamefanikiwa kupata wateja kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRCO, Comoro, Marekani, Uingereza, Sweden na mataifa mbalimbali ambao wamepata watoto na wanaendelea vizuri.

Ingawa kiwango cha mafanikio ya tiba hiyo kidunia huwa ni asilimia 45 mpaka 50, alisema Kairuki IVF imefikisha mafanikio ya kupata watoto kwa njia ya upandikizaji na kufikia wastani wa asilimia 63.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kairuki, Asser Mchomvu, alisema walipata wazo la kuanzisha kituo hicho baada ya kupata watu wengi wenye shida ya kupata ujauzito waliokuwa wanafika Hospitali ya Kairuki Mikocheni wakitafuta huduma hiyo.

Alisema wanawake wengi wamekuwa wakiteseka kwenye ndoa zao kwa kushambuliwa na ndugu, jamaa na marafiki inapotokea hajapata ujauzito wakati tatizo linaweza kuwa ni mbegu hafifu za mwanaume.

"Kwa utamaduni wa makabila mengi Afrika mtoto asipopatikana basi wanawake wamekuwa wakionekana kuwa ndiyo wenye matatizo lakini kwa uhalisia wakienda kupima wanaume wengi wanakutwa na tatizo hilo kwa hiyo sisi tuliliona tukaona tuanzishe kituo kumaliza tatizo hilo watu wapate watoto waishi kwa furaha," alisema.




Baadhi ya mamalishe wakishiriki shindano la msimu mpya wa mamalishe mwaka 2024, linaloandaliwa chini ya kampeni ya Mamalishe ya East Africa Television na Radio, katika viwanja vya Mwinyijuma, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam jana. Jumla ya mamalishe 10, walichuana huku mshindi mmoja akiondoka na zawadi kubwa ya kiwanja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BoT yaonya biashara ununuzi fedha chakavu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imewaonya watu wanaofanya biashara ya kununua fedha chakavu mitaani na kuwataka Watanzania kuwapuuza na kwenda katika taasisi za fedha ili kuzibadilisha.

Imesema benki zote za biashara zimepewa dhamana ya kununua na kuuza fedha halali na kwa thamani husika, hivyo wanaopita mitaani kununua wanakiuka sheria.

Kaimu Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sarafu wa BoT, Ilulu Ilulu, alisema hayo jana jijini Dar ea Salaam wakati akielezea mpango wa kuondoa noti za zamani kwenye mzunguko wa sarafu.

"Kuna watu wanapita mtaani na vi-spika (vipaza sauti) wanatangaza kwamba wananunua fedha chakavu. Kufanya hivyo ni kosa kisheria. Watanzania kama mna fedha chakavu nendeni benki za biashara mkabadilishiwe. Hao watu wananunua fedha chakavu kwa bei ndogo na kwenda kuuza kwa bei kubwa," alisema Ilulu.

Alisema taasisi za fedha zilizopewa dhamana ya kuuza kununua fedha zinamadirisha maalumu ya kupokea fedha za aina hiyo, kwamba wananchi wanapaswa kwenda. Kuhusu mchakato wa kuondoa noti za zamani kwenye mzunguko, Ilulu alisema Watanzania wasiwe na wasiwasi kwamba siyo mara ya kwanza kufanyika nchini.

Alisema BoT ilishawahi kufanya mchakato huo mara nne na sasa ni mara ya tano, akitolea mfano mwaka 1977 noti ya Sh.100 iliyochapishwa kuanzia mwaka 1966 mpaka mwaka 1977 iliondolewa katika mzunguko.

Alisema pia mwaka 1979 BoT iliendesha operesheni ya kuondoa noti ya Sh.10 na Sh. 20 zilizochapishwa kati ya mwaka 1966 mpaka mwaka 1979.

Ilulu alisema mwaka 1980 BoT iliendesha operesheni nyingine ya kuondoa noti ya Shilingi tano, Sh.20 zilizochapishwa kati ya mwaka 1966 mpaka mwaka 1980.

Kadhalika, alisema mwaka 1995 BoT pia iliziondoa noti ya Sh.50 na Sh.100 katika mzunguko zilizochapishwa kati ya mwaka 1979 mpaka mwaka 1995.

"Hivyo basi, BoT inapenda kuufahamisha umma kuhusu kuondoa kwenye mzunguko noti za zamani za Sh. 20, Sh.200, Sh.500, Sh.1,000, Sh.2,000, Sh.5,000 na Sh.10,000 kwa matoleo ya mwaka 1985 hadi mwaka 2003 na noti ya Sh.500 iliyotolewa mwaka 2010 zenye sifa zilizoainishwa kwenye Tangazo la Serikali Na.858 la Oktoba 2024," alisema.

Alisema utaratibu wa kuanza zoezi la kubadilisha noti hizo litaanza Januari 6, mwakani na kipindi cha miezi mitatu hadi Aprili.

# Angalizo latolewa ufugaji kuku katika vizimba

**Na Beatrice Shayo**

WAFUGAJI wa kuku nchini, hasa wanaotumia vizimba, wameshauriwa kuzingatia haki za ustawi wa wanyama wanapowafuga ili wapate soko ndani na nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Aneth Kitambi, wakati wa mafunzo yaliyolenga kuzingatia haki za wanyama kwa upande wa kuku na ndege wengine ambao wanafugwa.

"Tulikuwa tunaangalia madhara ya kuku kufugwa kwenye vizimba (Cages). Cages zipo za aina mbalimbali tumeona wakifugwa wengi sehemu moja wanaathirika kwa sababu hawazingatii ukubwa wa eneo na kusababisha madhara katika uzalishaji," alisema.

Alisema kuku aliyefugwa kwa vizimba thamani yake katika soko inauzwa bei ya chini ikilinganishwa na wengine wanaofugwa katika eneo kubwa wanajiachia na wanaweza kuruka na hata nyama yake huwa ina ladha nzuri.

Dk. Kitambi alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuendelea kufuga kwa kuzingatia ustawi wa wanyama ili wapate soko kwa wingi.

Aidha, alisema kuna maazimio waliyokubaliana ya muda mfupi na muda mrefu lengo kubwa ni kuhakikisha wafugaji wanazingatia haki za wanyama ikiwamo kuku na ndege wengine wanaofugwa.

Alisema sera na kanuni zao zipo vizuri ingawa kuna vipengele vichache ambavyo wanaendelea kuviongeza ili kuboresha sekta hiyo kwa kuwa masoko mengi yanataka kuzingatia haki za wanyama hao.

Aidha, alisema wataendelea kuwasiliana na balozi mbalimbali ili kupata masoko ambayo yanahitaji bidhaa zinazotokana na kuku wanaofugwa nje ya vizimba.

Alisema kwa Tanzania ufugaji wa vizimba bado ni mchache ni kati ya asilimia 10 hadi 20, hivyo kuku wengi wanafugwa kwenye maeneo mapana ndio maana watu wanapenda hiyo bidhaa.

"Rekebisho moja wapo ni kuhakikisha kuku wanaofugwa kwenye vizimba wanapunguza idadi na kuweka uwiano unaotakiwa badala ya kuwajaza wengi kwenye vizimba kufanya hivyo ni kuwanyima haki zao," alisema.

Mratibu wa Kituo cha elimu na ustawi wa wanyama kilichoko mkoani Dodoma, Ayubu Nnko, alisema kuna changamoto kubwa ya ufugaji wa kuku kwa kutumia vizimba kwa kuwa hawana uhuru hata wa kuruka na usalama wao upo hatarini.

Alisema wafugaji wengi wanakimbilia kufuga kwenye vizimba ili kurahisisha ufugaji bila kujali haki za ustawi wa wanyama hao.

"Kwenye hao kuku wa vizimba kunakuwa na magonjwa yanayosababishwa na mfumo wa hewa. Wafugaji wengi wanaofuga kwenye cage usafi wao ni duni jambo hilo serikali ilitizame kwa umakini," alisema.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, wakibadilishana nyaraka, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ushirikiano wa miaka minne ambapo benki hiyo itachangia kiasi cha Sh. bilioni moja kwa ajili ya matibabu ya watoto wenye matatizo ya moyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB kuchangia bil. 1/- gharama matibabu ya moyo watoto JKCI

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wametia saini makubaliano ya ushirikiano yatakayowezesha benki hiyo kusaidia gharama za matibabu ya watoto wanaotibiwa katika taasisi hiyo kwa kiasi cha Sh. bilioni moja kwa miaka minne sawa na Sh. milioni 250 kwa mwaka.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge mbele ya wanasheria wa taasisi hizo.

Akizungumza wakati wa utilianaji saini huo, Zaipuna alisema sekta ya afya ni miongoni mwa sekta za kipaumbele kwa taasisi yake ambayo inatambua na kuthamini juhudi kubwa zinazofanywa na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ambayo inachangia asilimia 70 ya matibabu ya watoto hao.

Alibainisha kuwa kwa mujibu wa makubaliano waliyotia saini, NMB inakwenda kusaidia asilimia 30 ya gharama za matibabu ambayo ni takribani Sh. milioni nne kwa mtoto mmoja, ambayo bado ni kubwa kwa wazazi na walezi wengi nchini kumudu kulipa na kuwezesha tiba kwa watoto wao.

"Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, zaidi ya watoto 13,800 huzaliwa na changamoto za moyo kwa mwaka hapa Tanzania, wengi miongoni mwa wazazi wa watoto hao wanashindwa kumudu gharama za matibabu, na hivyo watoto wengi huchelewa kupata matibabu stahiki na hivyo afya zao kuwa shakani.

"Sasa kwa makubaliano haya, NMB itachangia Sh. bilioni moja kwa kipindi cha miaka minne, ambapo kila mwaka tutachangia Sh. milioni 250 kuanzia mwaka huu na tuna imani mchango huu utakuwa msaada mkubwa hasa kwa wazazi wanaoshindwa kumudu gharama za matibabu ya watoto hawa," alisema.

Zaipuna alifafanua kwamba pamoja na mchango huo wa fedha taslimu, NMB pia itashirikiana na JKCI kuwezesha wataalamu wa magonjwa ya moyo wa taasisi hiyo kutoa elimu ya magonjwa ya moyo kwa wafanyakazi wa benki hiyo, wateja, pamoja na wadau wengine ili kusaidia kuongeza ufahamu wa afya ya moyo kwa Watanzania.

"NMB pia tutakuwa na wajibu wa kushiriki katika shughuli nyingine mbalimbali za kusaidia upatikanaji wa fedha zaidi zitakazowezesha matibabu ya watoto wanaotibiwa hapa kwa kushirikisha wadau wengine. Kwa hiyo, huu ni mwanzo tu wa ushirikiano huu wa NMB na JKCI," aliongeza.

Alipongeza JKCI na HTAF kwa kazi kubwa wanayofanya kwa watoto wa kitanzania na kwamba NMB inajivunia kuwa mshirika mkuu wa taasisi hizo mbili katika kutatua changamoto ya afya ya moyo na kurejesha tabasamu la watoto wenye maradhi hayo, huku akiwataka wadau wa afya nchini kuunga mkono jambo hilo.

Makubaliano haya ni mwendelezo NMB na taasisi za serikali, ambapo mwaka jana NMB ilifanya ukarabati mkubwa wodi ya wazazi ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), uliojumuisha pia uwekaji vifaa vipya na vya kisasa katika wodi hiyo iliyoko jengo ambalo sasa linaitwa Jengo la Uzazi la NMB.

Kabla ya kutia saini makubaliano hayo, Dk. Kisenge alishukuru NMB kwa kukubali kuingia makubaliano hayo, aliyoyataja yanakwenda kuunga mkono juhudi za Rais Samia, aliyempongeza kwa kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya afya nchini, hususani JKCI.

"Dk. Samia amefanya makubwa sana katika sekta ya afya na JKCI ni miongoni mwa wanufaika wa juhudi hizo, mapinduzi aliyoleta yanafanya JKCI kuwa taasisi kubwa na ya kwanza Afrika linapokuja suala la tiba za maradhi ya moyo, oparesheni salama na kuepusha vifo vitokanavyo na magonjwa ya moyo, ambavyo viko chini ya asilimia tano.

Alibainisha kwamba historia ya JKCI haiwezi kuelezwa popote bila kuitaja NMB, ambayo imefanya makubwa katika taasisi hiyo tangu mwaka 2015, ikisaidia si tu wagonjwa wanaotibiwa hapo, bali pia wafanyakazi wa taasisi kwa kuwapa huduma bora na rafiki, ikiwamo mikopo nafuu inayowaongezea ufanisi kazini.

"Kuthibitisha kuwa huu ni mwendelezo, mwaka 2017 NMB ilijenga eneo la mapumziko ya wagonjwa wa nje chini ya uongozi wa Prof. Mohamed Janabi, lakini mwaka 2022 wafanyakazi wa NMB walichanga sehemu ya mishahara yao kusaidia gharama za matibabu ya watoto waliofanyiwa upasuaji hapa.

"Mwaka 2023, Zaipuna alikuja hapa kushiriki Siku ya Wanawake Duniani, alitoa mchango mkubwa wa vifaa tiba, yakiwamo mashuka kwa wagonjwa, hii inaakisi ukweli kuwa NMB inajali wagonjwa, siyo tu wa hapa JKCI, bali sekta nzima ya afya nchini kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR)," alisema.

Dk. Kisenge aliahidi kwamba JKCI itazingatia makubaliano yaliyotiwa saini kuhakikisha kila mtanzania anapata elimu juu ya maradhi ya moyo, na wataendelea walipoishia kwa sababu tayari taasisi yake imeshazunguka katika mikoa 17, wataalamu wake wakionana na kusaidia zaidi ya wagonjwa 17,000.

"Nia ya ziara zetu mikoani ni kuwafikia waliko na kuwapunguzia mzigo wa kutufuata, tunaahidi ushirikiano mwema na NMB, ambao wateja wenye kadi za 'premium' za benki hii watatibiwa JKCI. Tunashukuru kwa namna NMB inavyojitoa kwa Watanzania, pia kwa jinsi inavyosaidia juhudi za Rais Samia," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Nusrati Hanje, akichangia hoja Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIMU JOSEPH**

# Mabilioni Mfuko wa Maji yatekeleza miradi 350

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Maji (NWF) umefanikisha ukamilishaji miradi ya maji 354 katika maeneo yenye uhaba wa huduma hiyo nchini kwa kipindi cha miaka mitatu.

Miradi hiyo imetekelezwa kupitia utaratibu wa mfuko huo kuzipatia mamlaka za maji mikopo ya masharti nafuu.

Hayo yalisemwa jana na Mtendaji Mkuu wa NWF, Haji Nandule wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu mafanikio waliyopata katika kipindi hicho cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni mwaka huu.

Nandule alisema kuwa miradi hiyo 354 ni kati ya miradi 998 iliyopokea fedha kutoka mfuko huo na kukamilika kwake kumenufaisha wananchi wapatao milioni 5.3 katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema miradi hiyo ilitekelezwa na mamlaka za maji mijini na vijijini baada ya kupata mkopo kutoka katika mfuko huo.

Mtendaji huyo alisema mfuko huo umekuwa ukitoa mkopo kwa mamlaka za maji kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na kusambaza huduma hiyo kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Nandule, hadi Julai mwaka huu, NWF ilikuwa imetoa mkopo wa Sh. bilioni 5.3 kwa mamlaka za maji nchini kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

Alisema mamlaka zilizokopeshwa ni zile zilizokidhi vigezo ikiwa ni pamoja na kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo iliyokopeshwa ili kuipunguzia serikali changamoto ya kupoteza fedha kutokana na kushindwa kulipa.

Alisema mfuko huo umekuwa unafanya hivyo ili kuzijengea mamlaka hizo uwezo wa kutekeleza miradi hiyo na kuwaondolea wananchi kero ya kukosa huduma hiyo.

Nandule alisema kwa sasa chanzo kikubwa cha fedha ni tozo ya mafuta ya petroli na dizeli Sh. 50 kwa kila lita inayouzwa katika vituo vya mafuta nchini.

Alibainisha kuwa kutokana na tozo hiyo, kwa mwaka mfuko huo unapata wastani wa Sh. bilioni 170.

Alivitaja vyanzo vingine vya fedha vya mfuko huo kuwa ni fedha zinazoidhinishwa na Bunge, misaada na michango ya fedha kwa mujibu wa sheria nyingine.

"Tozo hii ya Sh. 50 (kwa kila lita ya mafuta) inatozwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 16 ya Mwaka 2015," alisema Nandule katika kikao hicho ambacho ni kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa taasisi zilizopo chini yake kuelezea umma mafanikio na changamoto katika utendaji wa kazi.

Awali, Nandule alisema dira ya mfuko ni kutuma fedha kwa watekelezaji miradi ya usambazaji majisafi na ulinzi wa vyanzo vya maji nchini, pia kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji miradi ya usambazaji majisafi na ulinzi wa vyanzo vya maji.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prosper Buchakwe, alisema upotevu wa maji katika uendeshaji mamlaka za maji ni changamoto.

Buchakwe alisema changamoto hizo zinatokana na sababu mbalimbali, ukiwamo uchakavu wa miundombinu na wizi unaofanywa na watu wasiokuwa waaminifu.

"Kama maji yanavuja, jamii inatakiwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili wataalamu wafike kukagua na kutengeneza," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya NWF, Abdallah Mkufunzi, alisema majukumu ya mfuko huo ni kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maji, kufuatilia utekelezaji wake na kuzijengea uwezo mamlaka hizo kwa kuzipatia mikopo kwa masharti nafuu.

Mfuko huo ni taasisi ya fedha yenye lengo la kutoa fedha za utekelezaji miradi ya usambazaji majisafi kwenye maeneo yenye uhaba na utunzaji vyanzo vya maji nchini.

Uanzishwaji wake unalenga kuwa na chanzo cha fedha cha uhakika cha kutekeleza miradi ya maji nchini. NWF ilianza kufanya kazi rasmi mwaka wa fedha wa 2015/2016.

## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi ambao orodha yao ipo hapa chini waliolipia viwanja kwa nyakati tofauti eneo la Kikombo Kitalu "DA" na "N" kupitia benki, ila taarifa zao zinamapungufu ya majina, namba ya kiwanja na kitalu wafike ya Halmashauri iliyopo Manispaa ya zamani sehemu ya **mauzo ya viwanja** kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao.

Muda wa utekelezaji ni kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2024 hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

Kushindwa kufanya hivyo, umiliki huo hautatambulika tena.

**ORODHA YA MAJINA YENYE TAARIFA PUNGUFU**

| NA | JINA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher Kasung | 10,000.00 |
| 2. | Mbaga Iyombe | 1,000,000.00 |
| 3. | Veisi Maineko | 42,000.00 |
| 4. | George Abel Ngab | 300,000.00 |
| 5. | Ngalawe Hassan Ramadha | 6,931,641.00 |
| 6. | Esther Mpangala | 5,000,000.00 |
| 7. | Victoria Mgala | 400,000.00 |
| 8. | Godfrey K. Msongwe | 9,096,340.00 |
| 9. | Eliaza Mangera Wangwe | 5,148,000.00 |
| 10. | Florence N. Kebwe | 2,515,000.00 |
| 11. | Ali Hussein Habib | 338,300.00 |
| 12. | Joseph Lukumbika | 265,000.00 |
| 13. | Rosina J Delima | 2,249,554.00 |
| 14. | Kelvin Mlambalamba | 1,200,000.00 |
| 15. | Starphod Marwa | 1,000,000.00 |
| 16. | Ally H. Thabit | 3,000,000.00 |
| 17. | Mariam Tawakel | 10,000.00 |
| 18. | Jeremia Baha | 255,000.00 |
| 19. | Shani Mwaruka | 400,000.00 |
| 20. | Ramadhan N Simba | 50,000.00 |
| 21. | Ally Habiba Thabit | 3,000,000.00 |
| 22. | Job Ndalo | 100,000.00 |
| 23. | Giligoli A Ndaro | 100,000.00 |
| 24. | Gloria Reuben Ndaro | 80,000.00 |
| 25. | Magreth W Luma | 10,000.00 |
| 26. | Chedi Ng'enda | 21,729,382.00 |
| 27. | Sospeter N Marco | 2,500,000.00 |
| 28. | Geophrey Mtweve | 1,150,000.00 |
| 29. | Leonary Kimario | 24,000.00 |
| 30. | Lilian Sebastian | 1,625,000.00 |
| 31. | Anna Elisamehe | 400,000.00 |
| 32. | Olais Peter | 300,000.00 |
| 33. | Mussa Deogratius Limb | 4,566,560.00 |
| 34. | Marium | 225,000.00 |
| 35. | Rainer | 4,607,934.00 |
| 36. | George | 100,000.00 |
| 37. | Jafari | 500,000.00 |
| 38. | Dann | 10,000.00 |
| 39. | Victoria | 1,015,000.00 |
| 40. | Jona | 50,000.00 |
| 41. | Alvin | 677,100.00 |
| 423. | Christina | 700,000.00 |
| 43. | Tina | 100,000.00 |
| 44. | Doreen | 300,000.00 |
| 45. | Kelvin | 1,500,000.00 |
| 46. | Innocent | 1,000,000.00 |
| 47. | Mabrouk | 100,000.00 |
| 48. | SHM | 1,000,000.00 |
| 49. | Khadija | 500,000.00 |
| 50. | Jackline | 40,000.00 |
| 51. | Zubeda | 100,000.00 |
| 52. | Kelvin | 250,000.00 |
| 53. | Antony | 180,000.00 |
| 54. | Stanley | 3,500,000.00 |
| 55. | Kelvin | 250,000.00 |
| 56. | | 2,000,000.00 |
| 57 | | 220,000.00 |
| 58. | | 4,447,406.00 |
| 59. | | 2,000,000.00 |
| 60. | | 5,000,000.00 |
| 61. | | 1,566,355.00 |

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi mgumu unahitajika kwa mashirika, taasisi mizigo

**BUNGE** la Tanzania linaendelea na mkutano wake wa 13 jijini Dodoma ambao pamoja na mambo mengine, limepokea na kujadili uchanguzi wa taarifa za kamati za kudumu za bunge kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23.

Tayari Bunge limeshapokea na kujadili taarifa za Kamati za Hesabu za Serikali (PAC), Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC). Miongoni mwa mwambo yaliyojitokeza na kuonesha kuwakera zaidi wabunge ni kuendelea kuwapo kwa mashirika na taasisi za umma ambazo zinaendelea kuipatia hasara serikali.

Katika mjadala wa ripoti hizo juzi, wabunge walibainisha kuwa baadhi ya mashirika na taasisi yanajiendesha kwa ufanisi duni na kuendelea kutegemea ruzuku kutoka serikalini. Kutokana na hali hiyo, ilielezwa kuwa utegemezi wa mashirika na taasisi hizo umeongezeka kutoka Sh. bilioni 13.2 hadi bilioni 17.4.

Sababu kubwa zilizoelezwa na wabunge hao ambazo si ngeni kwa kuwa hata Msajili wa Hazina, amekuwa akieleza ni kuwapo kwa utendaji duni wa baadhi ya watendaji wakuu na maofisa waandamizi, ukosefu wa mitaji, tija ndogo na ufanisi. Sababu zingine ni kutokuwapo kwa mipango thabiti ya maendeleo na ya taasisi, uteuzi wa wajumbe wa bodi za wakurugenzi kufanyika kwa misingi ya kisiasa zaidi badala ya weledi, uwezo na taaluma pamoja na serikali kuziingilia bodi hizo katika majukumu yao.

Kutokana na kuwapo kwa tatizo hilo, baadhi ya wabunge waliochangia katika mjadala wa taarifa hizo za kamati walishauri serikali kuangalia wa kuyafunga, kuyafilisi au kuingia ubia na wawekezaji ili kuyaongezea ufanisi na kutengeneza faida.

Pia walishauri kwamba wanaoteuliwa kwenye uongozi wa taasisi hizo, wawe na uwezo, maarifa ya kazi wanazopewa. Kwa wajumbe wa bodi za wakurugenzi, wawe na uwezo na wasiteuliwe kwa misingi ya urafiki na kisiasa na pia wasipelekwe watu ambao ni wastaafu.

Kwa ujumla, kuendelea kuwapo kwa mashirika na taasisi za umma ambazo utendaji wao ni mbovu ni mzigo kwa serikali kwa sababu fedha hizo zingefanya shughuli zingine zingeleta matokeo chanya. Imebainika kwamba kati ya mashirika 35 ya kibiashara yaliyo chini ya serikali, 17 hayawezi kujiendesha, hivyo yanaendelea kupokea ruzuku kutoka Hazina.

Michango iliyotolewa na wabunge hao pamoja na ushauri vimeonesha dhahiri kwamba hawaridhishwi na hali ilivyo. Kwa mantiki hiyo, ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kuchukua hatua za haraka kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa ili kuleta ufanisi kwa mashirika na taasisi hizo.

Wakati wa mikutano ya watendaji wakuu na wenyeviti wa bodi za taasisi hizo, Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza kuwa serikali haiwezi kuyavumilia mashirika ya umma ambayo aliyaita mizigo kwa sababu kuendelea kuwapo kwao kunaongeza uzito katika kuyaendesha. Hata Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hivi karibuni kuwa hatua zinachukuliwa ama kuyafuta au kuyaunganisha baadhi ya mashirika.

Ni wazi kwamba hilo ni zuri na ziko hatua ambazo zilichukuliwa kwa utekelezaji wa jambo hilo. Kasi inatakiwa zaidi katika kuchukua hatua hizo na dawa pekee ni Bunge kufanya mabadiliko ya Sheria ya Msajili wa Hazina ili kuipa meno kuyasimamia mashirika hayo.

Aidha, kuwapo kwa ushindani katika uteuzi wa maofisa watendaji wakuu wa taasisi hizo, kutawezesha kuwapo kwa utendaji wenye matokeo chanya badala ya hali ilivyo sasa ya watu kuteuliwa bila kujua uwezo wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Bima Afya Kwa Wote kwa kaya maskini inakuja hivi...

Na Yasmine Protace

**TUNAPOZUNGUMZIA** kuhusu kaya maskini, tunagusa zile zenye umaskini wa kukithiri.

Ni lile kundi ambalo wanakwama kumudu matumizi ya milo mitatu kwa siku ikibaki kuwa bidhaa adimu kwao. Wao ni wa mlo mmoja kwa siku, tena unaopatikana kwa shida.

Nasema, kaya hizo zinakwama hata kuwapeleka watoto wao kliniki au shule. Uwezo wa kufanya hivyo nao unabaki kuwa bidhaa adimu.

Mavazi yakiwa ni lingine nyeti, ikiwamo hata katika orodha kitaifa kuhusu hadhi ya binadamu, kwa kaya hizo nguo za kuvaa ni changamoto, huku makazi wanayoishi nayo ni changamoto inayojitegemea.

Pamoja na kaya hizo kupitia magumu na mitihani hiyo, daima serikali yao imesimama katika ajenda ya kutowasahau watu wake. Serikali imeandaa utaratibu wa kuibuliwa kwa kaya hizo na kuziingiza katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF).

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Jenister Mhagama, akasema kuwa zaidi ya kaya milioni moja nchini Tanzania zitanufaika na mpango wa serikali wa kusaidia kaya zisizojiweza, ili ziweze kupata huduma stahiki za afya kupitia sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Mhagama anayasema hayo jijini Dodoma, wakati akiwasilisha taarifa ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Ameyasema hayo katika kikao na Kamati ya Bunge ya Huduma ya Afya na Masuala ya Ukimwi, chombo hicho kikiongozwa na Mwenyekiti Elibariki Kingu.

Akatamka: "Tanzania bara inajumla ya kaya milioni14.8 ambapo kaya milioni 3.9 ni kaya zisizo na uwezo."

Waziri huyo wa Afya, akaendelea kusema kuwa kuna kaya milioni 1.2, ambazo ni sawa na asilimia 32.3, serikali ikiwa imejipanga kuanza kugharamia Bima ya Afya kwa Wote kwa kundi hilo.

Anasema, kundi hilo litatambuliwa kama kaya zenye umaskini uliokithiri, zinazotambuliwa na mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF) unaohusika na kunusuru kaya masikini.

" Kifungu cha 25 Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura Namba 161, kimeanzisha mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo, ambao serikali imejipanga kuanza ugharamiaji wa Bima ya Afya kwa Wote," anatamka waziri.

Anasema kuna jumla ya kaya milioni 1.2 ambazo zimetambuliwa kuwa na kaya zenye umaskini uliokithiri.

Anaongeza kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali, ikijumuisha watoa huduma za afya na wadau wa maendeleo katika Sekta ya Afya.

Hapo kunalengwa kuhakikisha utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote

unafanikishwa kwa ufanisi, hivyo matarajio ni wananchi wasio na uwezo watanufaika na huduma hizo.

Waziri ana maoni kwamba wizara yake inazidi kuimarisha ubora wa huduma za afya katika vituo vya utoaji huduma hizo, akiwa ana uchambuzi wa namna hii:

Anatumia kauli: " Miundombinu inaboreshwa, upatikaji wa dawa vifaa tibà na vitendanishi ikiwamo uendelezwaji wa wataalamu na ubingwa bobezi."

Anaongeza kuwapo uimarishwaji kada mpya za tiba, pamoja na huduma za uzazi wa dharura na watoto wachanga (EMONC) katika ngazi ya msingi.

Mkurugenzi wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Dk. Irene Isaka, anasema wamejipanga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama, kwa kusimamia utekelezaji wa miongozo ya tiba.

Hapo kuna kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu mtindo bora wa maisha, lengo ni kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

# Wahukumiwa miaka 15 kwa ugaidi Tanzania, Msumbiji

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Masijala Ndogo Mtwara imewatia hatiani washtakiwa wanne na kuwahukumu kifungo cha miaka 15 gerezani kwa kosa la kula njama kufanya ugaidi Msumbiji na Tanzania.

Mahakama hiyo pia imemwachia huru mshtakiwa wa tano, Busra Ally baada ya kubaini upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yake.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi mbele ya Jaji Godfrey Isaya baada ya pande zote mbili kufunga ushahidi ambapo upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi 13.

Washtakiwa ni Ramadhan Makai, Abdulrazak Abdu 'Mnielewa Tunalapa', Rashid Kontola 'Liko', Salum Mnemba na Busra Ally aliyeachiwa huru.

Washtakiwa wote kwa pamoja katika shtaka la kwanza walidaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na shtaka la pili walituhumiwa kwa matumizi ya mali kwa ajili ya kutekeleza vitendo vya kigaidi.

> **"Yote yakizingatiwa, ninawahukumu kwa shtaka la kwanza, mshtakiwa wa 1, 2, 3 na 4 kifungo cha miaka 20 jela lakini kwa kuwa mmekuwa gerezani tangu mwaka 2017, mahakama inawapunguzia adhabu kila mmoja atatumikia kifungo cha miaka 15 jela.**

Katika shtaka la tatu, mshtakiwa wa tano alidaiwa kushindwa kufichua taarifa zinazohusiana na vitendo vya kigaidi, shtaka la nne kwa mshtakiwa wa pili ni matumizi ya mali kwa ajili ya kutekeleza kitendo cha kigaidi.

Katika maelezo ya awali, ilidaiwa kuwa washtakiwa hao kwa tarehe tofauti, walitenda makosa hayo kati ya Agosti Mosi 2017 na Oktoba 25, 2017 katika kijiji cha Tangazo, wilayani Mtwara Vijijini.

Baada ya kusomewa maelezo hayo ya awali, washtakiwa wote walikana kuhusika katika tukio hilo. Upande wa Mashtaka katika shauri hilo uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu Nassoro Katuga aliyesaidiwa na Cecilian Mkonongo, Basilius Namkande, Ester Martin na Timotheo Mmari.

Upande wa utetezi kwa nyakati tofauti uliwakilishwa na Makili Hussein Mtengwa, Rainery Songea, Happiness Sabato, Emmanuel Ngongi, Baraka Maugo, Hekima Mwasipu, Marietha Mollel, Adolf Runyoro, Mwanahamis Kilongo, Ole Mkulago na Juma Nassoro.

Mawakili wengine ni Abubakar Salim, Hamidu Ubaidi, Hamza Matongo na Adnani Chitale. Katika nia ya kuthibitisha kesi dhidi ya washtakiwa, upande wa mashtaka uliita mashahidi 13 na vielelezo vinane ambavyo mahakama hiyo ilikubali kupokea.

Vielelezo hivyo ni sanduku lenye visu vya kijeshi 96, gunia la mbolea ya urea ya buluu, sanduku lenye umbo la sitaha na jeli inayolipuka, hati ya ukamataji ya Oktoba 29, 2017, vilipuzi na maelezo ya onyo ya washtakiwa.

Jaji Isaya alisoma sehemu ya ushahidi wa upande wa mashtaka ambao ulidai washtakiwa walikuwa wamevaa magwanda na walifanya baadhi ya vitendo vya kigaidi.

Inadaiwa Jeshi la Polisi Tanzania lilikuwa na taarifa za kijasusi Oktoba 5, 2017 kwamba kulitokea matukio ya kigaidi yanayohusisha mashambulizi ya kigaidi Msumbiji ambapo kundi la kigaidi linalojulikana kama Al-Shabab lilihusika.

Katika ushahidi huo, inadaiwa baadhi ya wanachama wa Al-Shabab walihusika kuanza kuvuka mpaka wa Tanzania na kuelekea vijiji vya jirani vinavyopakana na Msumbiji na mkoa wa Mtwara.

Inadaiwa kulikuwa na wanajihadi walikuwa wakipanga kurusha vilipuzi na kuharibu majengo ya serikali, madaraja na vituo vya polisi vya Msumbiji na kununua silaha zaidi ili kupata nguvu Msumbiji na baadaye kuendeleza shughuli zao Tanzania. Inadaiwa katika ushahidi huo kuwa Al-Shabab Msumbiji walikuwa na uhusiano na familia moja au wakala kama kundi la wananchi wa Tanzania waliohama kutoka Kibiti, Ikwiriri, Mkuranga na Rufiji.

Shahidi wa kwanza upande wa mashtaka alidai kuwa mshtakiwa wa kwanza alikiri kuwasiliana moja kwa moja na mwanajihadi wa Tanzania, Seleman Mussa 'Nguvu' aliyekuwa anafanya shughuli zake Msumbiji.

Inadaiwa watuhumiwa walipokea shehena inayoshukiwa kuwa vilipuzi kwa shughuli za kigaidi.

Baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili, mahakama iliamua kumwachia huru Busra Ally kwa sababu upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashtaka katika shtaka la kwanza dhidi yake.

Mahakama iliwatia hatiani mshtakiwa 1, 2, 3 na 4 kwa shtaka la kwanza la kula njama kufanya ugaidi.

"Katika kutoa adhabu, nimezingatia maombolezo kutoka pande zote mbili. Kweli makosa yalifanywa yanaweza kuleta athari mbaya kwa watu wote nchini kwa sababu ya vitendo vya ugaidi na machafuko yanaathiri uchumi wetu na mpangilio wa kijamii wa jamii.

"Vitendo hivi vinaweza kuharibu uhusiano mzuri tulionao na nchi nyingine, nimezingatia vipengele vya kupunguza adhabu vilivyoendelezwa, ninakubali washtakiwa wamekaa gerezani kwa muda mrefu sana.

"Yote yakizingatiwa, ninawahukumu kwa shtaka la kwanza, mshtakiwa wa 1, 2, 3 na 4 kifungo cha miaka 20 jela lakini kwa kuwa mmekuwa gerezani tangu mwaka 2017, mahakama inawapunguzia adhabu kila mmoja atatumikia kifungo cha miaka 15 jela.

"Mahakama inaamuru vielelezo viharibiwe na kabla ya utekelezaji viwe chini ya ulinzi wa polisi," hukumu ilitolewa.


SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
MAMLAKA YA USAFIRI WA BAHARINI ZANZIBAR (ZMA)

**Salaam za Pongezi**




**Dr. Hussein Ali Mwinyi**
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA) inaungana na Wazanzibari wote katika kumpongeza Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Dkt. Ali Hussein Mwinyi** katika kuadhimisha Miaka Minne ya uongozi wake visiwani.

**Tunamtakia Kila la kheri katika utekelezaji wa Majukumu yake.**

**"Usalama na Maendeleo ya Bahari Yetu"**

S.L.P 401, Malindi-Zanzibar
Baruapepe: info@zma.go.tz , Tovuti: www.zam.go.tz
Simu: +255 24 2236795



Zanzibar Insurance Corporation
SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR (ZIC)

**HONGERA KWA KUTIMIZA MIAKA 4 OFISINI**

MIAKA MINNE YA DK. MWINYI



*Dr. Hussein Ali Mwinyi*
*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi*

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) inaungana na Wazanzibar wote katika kumpongeza Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Hussein Mwinyi katika kuadhimisha Miaka Minne ya uongozi wake visiwani.

Tunamtakia Kila la kheri katika utekelezaji wa Majukumu yake.

**"Uhakika na Usalama kwa Kila Hatua"**

4 MIAKA OFISINI

HEAD OFFICE; (Maisara) Mpirani P.O.Box:432, Zanzibar Tel:+255 24 2232676 / 2233867 /2239504 Fax: +225-24 2232422 Email: zichq@zic.co.tz

LAKE ZONE (MWANZA) Alpha Building, 2nd Floor, P.O. Box: 829, Mwanza Tel: +255-28 2500168, Fax: +255-282500410 Email: zicmwa@zic.co.tz

COASTAL ZONE (DARES SALAAM) Lumumba/ Morogoro Road Opp. Vijana Building Plot No. 65, 3rd Floor PO. Box: 8631. Dar es salaam Tel: Direct: +255-22 2183161/2181993 Tel: General: +255-22 2183561/2182639 Fax: +255-22 2183562, Email: zicdsm@zic.co.tz

CENTRAL ZONE P.O. Box 4488 Tel: +255 26 2320063, Fax: +255 26 2320064

SOUTHERN HIGHLAND P.O.Box: 324, Wete - Pemba Tel/Fax: +255-24 2452151 Email: zicpba@zic.co.tz

## MATANGAZO


MIAKA MINNE YA DK. MWINYI 4

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
**UTALII NA MAMBO YA KALE ZANZIBAR**

SMZ SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

# SALAMU ZA PONGEZI
## KWA KUTIMIZA MIAKA 4 OFISINI

Viongozi na wafanyakazi wa wizaya Utalii na Mambo ya Kale inaungana na Wazanzibar wote katika kumpongeza Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Hussein Mwinyi katika kuadhimisha Miaka Minne ya uongozi wake visiwani.

Tunamtakia Kila la kheri katika utekelezaji wa Majukumu yake.



*His Excellency The President of the Revolutionary Government of Zanzibar, Dr. Hussein Ali Mwinyi*

**Mawasiliano**
Mnazi Mmoja, Zanzibar
S.L.P 22277, Zanzibar
Baruapepe: info@utaliismz.go.tz
Tovuti: www.utaliismz.go.tz



MIAKA MINNE YA DK. MWINYI 4

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
**SHIRIKA LA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)**

ZANZIBAR SOCIAL SECURITY FUND ZSSF Key to the Future

# Salamu za Pongezi

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) inaungana na Wazanzibar wote katika kumpongeza Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Hussein Mwinyi katika kuadhimisha Miaka Minne ya uongozi wake visiwani.

**Tunamtakia Kila la kheri katika utekelezaji wa Majukumu yake.**

**"zssf kwa maisha ya sasa na baadae"**



**Dr. Hussein Ali Mwinyi**
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

MIAKA **4** **OFISINI** ya kishindo

**Afisi Kuu Mnara wa Mbao, Zanzibar Nambari:+255 24 2452050 +255 24 2232820, Baruapepe: info@zssf.or.tz, Tovuti: www.zssf.or.tz**

# Wagombea wabebeshwa zigo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKAZI wa Kata ya Pasua Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro wamewataka wagombea uenyekiti mitaa, vijiji na vitongoji kuhimiza serikali kuyainua kiuchumi makundi maalumu wakati wa kijinadi kwa wananchi katika mikutano ya kampeni inayoanza Novemba 20, mwaka huu.

Wakazi hao wanataka wagombea hao kuhubiri namna wanavyoweza kuchochea kuinua kipato kupitia uwekezaji katika miradi midogo ya kiuchumi katika maeneo yao.

Akizungumza jana na vikundi vya Kwa Mkoyi Vikoba, Tumaini Group na Matunda Vikoba Group, wakati wa kikao kazi cha wadau wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT), Immaculatha Mwigani, alisema baada ya serikali kurejesha mikopo ya asilimia 10, Julai mosi mwaka huu, wanataka sera hiyo ya mikopo iwe na tija kwa kila mwananchi.

"Pasua tuna changamoto nyingi za huduma za afya, elimu na masuala ya ukatili kama ulawiti kwa watoto wa kiume na ubakaji kwa wanawake na watoto. Tunataka wagombea wetu katika uchaguzi huu wa serikali za mitaa wahubiri haya, waonyeshe namna watakavyoyakabili," alisema na kuongeza: "Vilevile watembee na ajenda yetu ya kuboreshwa vikundi vyetu vya kiuchumi. Kwa sababu ili kuinua kipato kupitia uwekezaji katika miradi midogo ya kiuchumi, serikali na wananchi wanaweza kutoa elimu na mafunzo, kwa kuandaa programu za mafunzo kwa wananchi kuhusu usimamizi wa miradi, ujasiriamali na ufundi."

> **"Tumekuwa tukilaumu kiongozi fulani labda ameingia madarakani, tunasema huyo bwana hatufai, huyu sijui nini lakini inawezekana yuko mama mwenye sifa zake, angeweza kujitokeza na akapata**

Mwenyekiti wa Matunda Vikoba Group, Amina Hussein, alisema wanachotaka serikali ikifanye na wagombea wao waahidi kuvisimamia, ni hoja ya kupunguza vikwazo vya kisheria ili kurahisisha taratibu za kuanzisha biashara na kutoa leseni kwa urahisi.

Amina, alisema vingine ni kuwezesha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuboresha mazingira ya biashara. Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, Veronica Ollomi, alisema lengo la mradi huo kuhamasisha wanawake wenye sifa, nia na kiu ya kugombea uongozi.

"Tumekuwa tukilaumu kiongozi fulani labda ameingia madarakani, tunasema huyo bwana hatufai, huyu sijui nini lakini inawezekana yuko mama mwenye sifa zake, angeweza kujitokeza na akapata nafasi hiyo ambayo ingekuja kuwasaidia kuepeka ajenda za kinamama katika ngazi za juu zaidi na kutatua zile kero za kinamama," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, Wizara hiyo tayari imesanifu na kujenga mfumo wa 'Wezesha Portal' utakaotumika kutoa mikopo hiyo.

Mchengerwa, alisema mfumo huo utasaidia kuondoa changamoto za awali, ikiwamo vikundi hewa, watu kujisajili zaidi ya kikundi kimoja na wakopaji hewa.

Alisema mfumo huo utaimarisha usimamizi, usajili wa vikundi, utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo na upatikanaji wa taarifa sahihi za mikopo kwa wakati ili kuongeza tija, kuondoa upendeleo na kuongeza uwazi na uwajibikaji.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainab Abdallah, akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Lishe, iliyofanyika kiwilaya katika Shule ya Msingi Kwamkabara, juzi. Wengine ni Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Fani Mussa (kulia), Diwani wa Kata ya Kwamkabara, Peter Mgavilwa (wa tatu kulia) na (kushoto) ni Katibu Tawala, Mohamed Mfaki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Siri mitaji ya wajasiriamali kufa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WAZALISHAJI wa mazao ya kilimo ikolojia nchini wamesema mitaji ya baadhi ya wajasiriamali inakufa, kukosa tija na ufanisi kutokana na matumizi duni ya teknolojia na gharama kubwa.

Akizungumza jijini hapa wakati wa mafunzo ya kujenga uwezo kwa vijana katika mifumo ya chakula, Micky Lucas kutoka Taasisi ya Arusha Food Systems Youth Leaders, alisema kitu kingine kinachokwamisha wajasiriamali hao katika miradi ya ufugaji, uvuvi na kilimo ni matumizi ya teknolojia duni.

'Mimi ni mdau wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Kuna vitu vinasababisha uzalishaji usiendelee kuwa endelevu. Mojawapo ni suala la teknolojia; kwamba ni vitu gani vinaweza kufanya uzalishaji kwa njia ya teknolojia kuwa nzuri," alisema.

Ofisa Vijana wa Shirika la Global Alliance for Improved Nutrition (gain), Saddam Halfan, alisema vijana hao wamekutana katika mkutano ambao ni sehemu ya utekelezaji wa kipengele cha kuwajengea uwezo katika mifumo ya chakula, unaotokana na Mradi wa NFP.

"Tunajadiliana kwa pamoja, ni nini ambacho wao wanaona kinafanyika katika mifumo ya chakula, na kipi ambacho wao wanaona kifanyike kama vijana, ambao ni wanufaika wakubwa wa mifumo ya chakula, kuifanya iwe jumuishi na endelevu," alisema. Mradi wa Nourishing Food Pathway (NFP) unatekelezwa na Global Alliance for Improved Nutrition (gain) kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Uingereza na wadau wengine kutoka taasisi binafsi.

# Watakiwa kuchangamkia nembo ya ubora TBS

**Na Joseph Mwendapole,** MANYARA

SHIRIKA la Viwango Nchini (TBS) limewataka wazalishaji wa bidhaa nchini kutafuta nembo ya ubora ili wapate kibali cha kufanya biashara kwenye masoko ya nje ya Afrika Mashariki.

Rai hiyo imetolewa na Meneja wa TBS Kanda ya Kaskazini, Joseph Ismail, wakati akizungumza katika maonyesho ya Chama cha Wenye Viwanda, Biashara na Kilimo (TCCIA) yanayoendelea katika Wilaya ya Babati, mkoani hapa.

Ismail, alisema serikali imeamua kuwaita mezani wazalishaji wote ili kurasimisha bidhaa zao.

"Waje kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha ili waweze kuuza nje ya Soko la Afrika Mashariki na kupata mikopo kwenye taasisi za fedha. TBS wanaingiaje kwenye uwekezaji, ni kwa sababu wanawezesha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali," alisema.

Aliwataka wazalisha kurasimisha biashara zao kwani baada ya kupata nembo ya ubora wa shirika hizo, wataweza kuuza bidhaa zao nje ya Afrika Mashariki.

Alitoa mfano kwa kusema Manyara ni mkoa wa kimkakati wenye hoteli nyingi, lakini hazwezi kununua bidhaa zisizokuwa na nembo ya TBS.


"Kwa hiyo ili uweze kuuza kwenye hoteli hizo ni lazima uthibitishe ubora wa bidhaa zako. Wenye hoteli badala ya kwenda kununua bidhaa Arusha watanunua Manyara, lakini hawawezi kununua bidhaa Manyara ambazo hazijathibitishwa ubora wake na TBS," alisema Ismail.

Alisema TBS ni taasisi rafiki ambayo ipo karibu na wajasiriamali, ambapo serikali inatenga fedha kwa ajili ya kuhudumia wajasiriamali.

"Kwa hiyo serikali kupitia TBS inatoa huduma hiyo ya kuthibitisha ubora wa bidhaa za wajasiriamali pasipo kulipia gharama zozote," alisema na kusisitiza:

"Kuthibitisha kuna gharama, lakini serikali kupitia TBS inatoa huduma hizo bure, kwa hiyo natoa hamasa kwa wajasiriamali waje TBS waweze kuthibitisha bidhaa zao," alisema.

Maonesho hayo yanaongozwa na kauli mbiu isemayo, 'Manyara kwa Ustawi wa Biashara na Uwekezaji.'





# Mfanyabiashara adaiwa kutekwa na wasiojulikana

**Na Samson Chacha,** TARIME

MFANYABIASHARA Joseph Mwita (50), mkazi wa Tarime mjini mkoani Mara, anadaiwa kutekwa na watu wasiojulikana waliomchukua na kumwingiza katika gari aina ya Toyota Hard Top na watu wasiojulikana majira ya saa tatu usiku na kutoweka naye.

Mfanyabiashara huyo anadaiwa kuchukuliwa na watu hao waliokuwa na silaha za moto wakati akitoka kuchukua dawa kwenye duka nje ya stendi ya magari mjini hapa.

Akisimulia tukio hilo kijana wa mfanyabiashara huyo, Ibrahim Jumanne, alisema lilitokea wakati wakitoka katika mazishi ya mmoja wa madereva wilayani hapa yaliyofanyika huko Msati, Kata ya Nkende majira ya saa mbili usiku.

"Nilikuwa mimi na baba tukirudi nyumbani tulichukua bodaboda na baba alihitaji kupitia dawa dukani nje ya stendi ya magari na tupofika hapo baba alienda dukani na kuchukua dawa, wakati anavuka barabara tukapande pikipiki ndipo walipomkamata na kumwingiza katika gari aina ya Toyota Hard Top lenye rangi kama ya kijani na nyeusi watu wakiwa na silaha za moto," alisema Jumanne.

> **"Hii inathibitisha hali halisi ya maradhi yasioambukiza na uwapo wa haja ya kushirikiana kuongeza juhudi katika mapambano ya maradhi haya nchini mwetu," alisema.**

Aidha, alisema baada ya kushuhudia tukio hilo alijaribu kupiga yowe kuomba msaada bila mafanikio na kisha gari hilo kutoweka naye kusikojulikana.

Ibrahim alidai gari ilikuwa linawafuatilia wakati wakitoka msibani na kisha kusimama mbele yao na walishuka watu watano kutoka ndani ya gari hilo wakiwa na silaha za moto na kumwamuru baba yake kupanda ndani.

"Alikataa kupanda hivyo wakalazimika kumkamata kwa nguvu na kumpandisha ndani ya gari huku akipiga kelele kuomba msaada na mimi nilianza kupiga yowe kuomba msaada na baba yangu watu walijaribu kujitokeza kutaka kutoa msaada, lakini tulitishiwa na wale watu kwa silaha na gari likaondoka naye ghafla na kuelekea barabara ya Bomani," alisema.

Alisema baada ya tukio hilo aliwapigia simu ndugu akiwamo Maiko Mtiba, ambao walifika haraka na kuanza kufuatilia na kupiga simu kwenye kizuizi cha Polisi Komaswa na daraja la Kirumi na kutoa taarifa Kituo cha Polisi Tarime ili kupata msaada, lakini hawakufanikiwa.

Aidha, aliliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia kumpata baba yao au kujua alipo na kuwa hata kama ana makosa anayotuhumiwa nayo wafahamu alipo licha ya kutoa taarifa kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa pamoja na Kamanda wa Polisi mkoa, bila mafanikio.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya, SAPC Michael Njera, alithibitisha kupokea taarifa za tukio hilo na kuwa wanaendelea na uchunguzi kwa kuwa hawakuwa na taarifa zake hapo awali.

"Tumepokea taarifa hizo za kupotea kwa Joseph Mtiba kutoka kwa vijana wake Ibarahim na Maiko, suala hili tunalifanyia uchunguzi zaidi kwani hatukuwa na taarifa zake, tumewaambia hawa vijana Ibrahim na mwenzake Maiko wafungue jalada kisha tutalifanyia uchunguzi kwani hapa kwetu Tarime/Rorya hakuna mtu huyo anayeshikiliwa," alisema Kamanda Njera.




Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, Mohamed Mtulyakwaku (aliyesimama), akizungumza wakati akizindua ugawaji wa hati za hakimiliki za kimila zaidi ya 1,300 kwa wakazi wa vijiji vya Seki na Buduba, katika Halmashauri ya Wilaya hiyo, juzi. **PICHA: HALIMA IKUNJI**

# Wananchi 1,300 wapatiwa hatimiliki za ardhi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

SERIKALI kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Bora ya Ardhi (NLUPC ), imetoa hati za hakimiliki za kimila za ardhi kwa wananchi 1353 wa vijiji vya Seki na Buduba, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega mkoani Tabora ili kudhibiti migogoro ya ardhi baina ya vijiji na vijiji pamoja na wananchi kwa wananchi hasa wafugaji na wakulima.

Akizungumza juzi wakati wa ugawaji wa hati za hakimiliki za kimila za ardhi katika kijiji cha Seki, Kata ya Mwamala, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega mkoni hapa, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Mohamed Mtulyakwaku, alisema licha ya kudhibiti migogoro zitawasaidia pia kuwainua kiuchumi.

"Kupitia hati hizi wanaweza kupata mikopo kirahisi kutokana na kuwa na maeneo yaliyopimwa pamoja na hati za hakimiliki za maeneo hayo," alisema Mtulyakwaku.

Alisema kati ya hati hizo zilizotolewa, Kijiji cha Buduba zimeandaliwa hati 654 na Kijiji cha Seki zimeandaliwa hatimiliki 699.

Ofisa Ardhi Mkuu kutoka NLUPC, Otmary Komba, alisema lengo la uandaaji wa mpango huo ni kuondoa miingiliano ya kimatumizi ardhi katika vijiji vyenye migogoro na vilivyo pakana na nchi jirani.

Komba, alisema tume imefanya utatuzi wa migogoro katika vijiji hivyo kwa kupima mipaka ya maeneo yao pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi bora ya ardhi.

Baadhi ya wakazi wa vijiji hivyo akiwamo Nkwabi Maganga, walisema kupata hati hizo ni jambo litakalowasaidia kuondoa migogoro ya ardhi iliyokuwa ikiwakumba kabla ya kupimiwa kwa maeneo yao na kupewa hati za hakimiliki.

# Polisi wakopeshwa bil. 600/- kupitia SACCOS

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WATUMISHI kutoka Jeshi la Polisi nchini wametajwa kukopeshwa zaidi ya Sh.bilioni 561.7 katika kipindi cha miaka 18 kupitia ushirika wa kuweka akiba na kukopa wa Usalama wa Raia Savings and Credit Cooperative Society (URA SACCOS) ili kukidhi mahitaji yao na kudhibiti vitendo vya rushwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Ally Gugu, akizungumza juzi wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 16 wa ushirika huo uliofanyika mkoani Mwanza alioutaja kuwa chachu ya kurahisisha utendaji kazi kwa polisi.

Alisema tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006 mikopo 137,871 ya Sh. 561,701,776,822 imetolewa kwa wanachama hadi kufikia Septemba 30, 2024 ikiwa na masharti nafuu kulinganisha na taasisi nyingine za kifedha kwa lengo la kuboresha ustawi wao wa kiuchumi.

Gugu alisema wanachama wamezidi kuongezeka kutoka 4,300 wakati wa kuanzishwa hadi 48,001 na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuimarisha sekta hiyo kwa kuwekeza mtaji wa Shilingi bilioni tano ili kuimarisha huduma za kifedha kwa watumishi wote, ikiwamo Jeshi la Polisi.

Naye Kamishna wa Utawala na Rasilimali Watu Jeshi la Polisi, CP. Suzan Kaganda ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya URA SACCOS, alisema mafanikio ya ushirika huo yanachangia ukuaji wa Pato Ghafi la Taifa (GDP) kutokana na zaidi ya asilimia 75 ya mikopo iliyotolewa kuelekezwa katika ujenzi wa makazi binafsi ya wanachama na kuchangia katika mzunguko wa fedha na ukuaji wa uchumi wa kitaifa.

Mjumbe wa mkutano huo kutoka Masasi, mkoani Mtwara, Rodrique Mwangungulu, alisema ushirika huo unawasaidia kujiwekea akiba na kuwataka polisi wengine wachangamkie fursa hiyo na kujiunga ili waweze kufanya kazi bila mawazo.



Ukurasa 12

MAISHA YA MSTAAFU MSUGURI...

**Wakawa wanakijiji shambani na Nyerere, alipokuwa mwenyekiti, akawapa makubwa**




Ukurasa 13

Majina ya watu mashuhuri yanapogeuka shubiri kwao



Ukurasa 14

**Wajerumani na wana - Namtumbo walipoingia ubia kumaliza kasoro**


# BUFE

IJUMAA NOVEMBA 1, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


KILIO UVAMIZI TEMBO KUSINI...

# Agizo lake Rais Septemba hitaji la 'ndege nyuki', TAWA wameanza

**Na Mwandishi Wetu**



Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mabula Nyanda. **PICHA: MTANDAO**

MIKOA kadhaa nchini na wilaya zake zikiwamo Liwale na Nachingwea (Lindi), pia Tunduru ya Ruvuma, ambazo ziko katika ukanda mmoja, kuna historia ya suala la uvamizi wa tembo mashambani na makazi ya watu limezidi.

Inaelezwa hali hiyo yenye kipindi kirefu, mathalan Nachingwea ni mwaka wa tatu sasa, inaathiri usalama wa makazi na uzalishaji mashambani, pia kukwama. Agosti mwaka jana ilitoa sauti ya kifo huko Nachingwea, hata kuvuta hisia za kitaifa, huku Mkuu wa Wilaya hiyo, Mohamed Moyo, akiripotiwa ahadi yake serikali ingetumia ndege za helikopta kuwafukuza.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa ziarani wilayani Tunduru mwezi uliopita, sauti hiyo ya kilio cha uvamizi wa wanyama waharibifu akawasilishiwa tena, hata akaielekeza Wizara ya Maliasili kuongeza ndege nyuki (drones) kutekeleza kazi hiyo.

Akizungumza na wananchi wa Tunduru kwa nyakati tofauti katika ziara yake ya siku ya nne mkoani Ruvuma, Rais Dk. Samia akataja mikakati inayofanyika inajumuisha kuongeza askari wa wanyamapori na kuwaongezea ujuzi walioko vijijini, ili washirikiane kuwadhibiti tembo.

Akasema, serikali imeweka magari ya doria katika maeneo mbalimbali wilayani, kurahisisha shughuli hiyo, pia ndege nyuki ya kufukuza tembo, hatua inayofika pia wilayani Namtumbo.

"Tunajua kuna tatizo la tembo, lakini tumeanza kuchukua jitihada hizo na mengine yanafuatia, lengo letu ni kuongeza idadi ya ndege nyuki ili kufukuza tembo na kuimarisha vituo vya askari wa maliasili," akasema Rais Dk. Samia, mkutanoni katika uwanja wa Majimaji mjini Songea.

## WATEKELEZA MAAGIZO

Ni wastani wa wiki mbili na nusu baadaye (Oktoba 15), hatua za kiserikali zikaanza kushuhudiwa, pale Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mabula Nyanda, anapotangaza hatua kadhaa kukabili wanyamapori wakali na waharibifu, hususan tembo katika mikoa ya Ruvuma na Lindi.

Hivi sasa, serikali kupitia TAWA imetenga bajeti ya kwa ajili ya kununua ndege nyuki nne aina ya DJI Mavic 3 zitakazopelekwa wilayani Namtumbo (Ruvuma) na Liwale, Nachingwea na Lindi mkoani Lindi.

Kamishna Mabula, anayasema hayo mbele ya anayeongoza Kamati ay Ulinzi na Usalama, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ikiwa ni utakelezaji wa maelekezo ya Rais Dk. Samia, aliyoyatoa mkoani humo Septemba 28, 2024 kuhusu udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu katika wilaya za Namtumbo na Tunduru.

Mabula anasema katika mwaka wa fedha uliopo 2024/25, TAWA inatarajia kuajiri askari 351 watakaopangiwa vituo vilivyoko kwenye maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori hao.

Pia anataja, kuna askari 20 watapangiwa katika kituo kidogo cha Songea na watafanya kazi katika wilaya za Tunduru na Namtumbo, kunakotajwa kuwa na changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Vilevile, Kamishna Mabula anasisitiza TAWA inatarajia kununua gari moja na pikipiki mbili zitakazopelekwa katika kituo kidogo cha Songea, kutumika kudhibiti changamoto ya wanyamapori wilaya za Tunduru na Namtumbo.

Pia, anasema mamlaka tajwa itaboresha kituo kimoja cha Askari cha Kudumu katika wilaya ya Tunduru, pia vikosi viwili vya kudumu vya askari kutoka kituo kidogo cha Songea, ili kurahisisha mwitikio wa haraka wa matukio ya tembo.

Anasema, baada ya changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu kuwa endelevu, Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa mkakati wa kukabiliana na migongano hiyo, baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

Ni mkakati anaoutaja kutekelezwa na taasisi za wizara zilizo chini ya Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu (TAWA, TANAPA, NCAA na TFS) kwa kugawana maeneo, halmashauri za wilaya, taasisi zisizo za kiserikali, wadau wa uhifadhi na wananchi kwa ujumla.

## BUSTANI WANYAMAPORI

Aidha, Kamishna Mabula anasema, kuwapo bustani ya wanyamapori (zoo) hai inayosimamiwa, huko Ruhila katika Manispaa ya Songea, ikitajwa ni kivutio kwa wakazi mkoani humo, Kamishna Mabula amemwomba Mkuu wa Mkoa - Kanali Ahmed kusaidia ujenzi wake kiwango cha lami urefu wa kilomita tano kufika mahali hapo, kukiwa kivutio cha utalii.

Kanali Ahmed anapongeza Kamishna Mabula, kuzingatia na kutekeleza maagizo ya Rais kwenye ziara yake mkoani humo, mwezi uliopita.

Mkuu wa Mkoa, pia anasema jitihada za TAWA zinahuisha matumaini ya wananchi wa Ruvuma, kwa kuwa zinalenga kuimarisha usalama wa maisha na mali zao, dhidi ya uvamizi wa wanyamapori kwenye maeneo yao.

BIASHARA

MAISHA YA MSTAAFU MUSUGURI...

# Wakawa wanakijiji shambani na Nyerere, alipokuwa mwenyekiti, akawapa makubwa

• Siri ya mafanikio yake 'mtindo wa maisha' • Aligoma kuonana na mtoto wa Iddi Amin • Dar, waliovamia kwake, akawagawia viwanja

**Na Sabato Kasika**

NI msiba mkubwa unaobeba sura ya kitaifa na kihistoria, Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali David Musuguri anayetarajiwa kuzikwa Jumatatu wiki ijayo kijijini kwao Butiama, alikokuwa anaishi maisha yake ya ustaafu kwa miaka 36.

Uzalendo wake unatolewa mfano kila kona, ikiwamo kutoka kwa Mkuu wa Majeshi Mwasisi wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) mwaka 1964, Jenerali Mirisho Sarakikya.

Daima kabarikiwa kuishi umri miaka 104, akibaki na wasifu wake wa uzalendo na mtu wa watu, saa akishuka ngazi ya kijiji hasa.

Makazi yake ya ustaafu walishi kijiji kimoja na baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, yeye akimtangulia kiumri kwa miaka miwili na baada ya kustaafu walikuwa majirani kijijini, makazi yake na Nyerere wanatenganishwa na bonde fulani.

Hali ilivyo msiba wake wa leo, pia unawakumbusha wana Butiama, Mara, ugeni wa umati unaofika kwao kumuaga Mtanzania mwingine mzalendo aliyewatoka.

Ndio hali iliyotawala kwake Dar es Salaam, Mbezi kwa Msuguri, ukiwa ni ushuhuda wa Nipashe na taarifa kutoka kijijini Butiama, huku pilika za kitaifa ni nyingi, ratiba ya leo ya mazishi, Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko anatarajiwa kuongoza utoaji wa heshima za mwisho kabla ya mwili kusafirisha kwenda Butiama.

Katika zama za uongozi wake 1980 hadi 1988, Jenerali Musuguri na viongozi wenzake wa juu kabisa jeshini watatu kuna wakati walijulikana kwa umaarufu wa masihara MML; kwa maana ya Musuguri, Meja Jenerali Martin Mwakalindile na Meja Jenerali James Luhanga.

### KUTOKA BUTIAMA

Staili yake ya maisha kijijini inatajwa ni ileile ya mstaafu Nyerere, alivyoamua kurudi kuwa mkulima wa kawaida, miaka minne Nyerere akajikuta anamkaribisha Mkuu wa Majeshi mstaafu aliyesaidia ulinzi wake, pia kumtokomeza Adui Nduli Iddi Amin, wanaofahamiana vema, maana inaelezwa kihistoria walishahudhuria kozi za kijeshi pamoja.

Nipashe imezungumza na Katibu wa Ukoo wa Nyerere aliyejitambulisha kwa jina la Maghembe Jackton, anasema Musuguri amewahi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Butiama kwa muda wa mwaka mmoja.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakati akiwa Makamu wa Rais, alipomtembelea marehemu Jenerali Mstaafu David Musuguri, nyumbani kwake kijijini Butiama, Mara. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Baada ya kustaafu, Musuguri, alirudi hapa Butiama, baada ya miaka michache akawa Mwenyekiti wa Kijiji kuanzia mwaka 1990 hadi 1991.**

"Baada ya kustaafu , Musuguri, alirudi hapa Butiama, baada ya miaka michache akawa Mwenyekiti wa Kijiji kuanzia mwaka 1990 hadi 1991," anasema Jackton.

Pia, anasema, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, alimpendekeza ashike nafasi kwa muda mfupi kijijini, kabla ya uchaguzi, alipoona kijiji cha Butiama kinayumba kwa kukosa uongozi.

"Awali kijiji kilikuwa kinaongozwa na Joseph Nyerere (mdogo wa Mwalimu Nyerere) ambaye aliacha nafasi hiyo kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wake, hivyo kijiji kukosa mwenyekiti," anasimulia.

Katibu huyo wa Ukoo wa Nyerere, anasema mazingira hayo yalimfanya Baba wa Taifa amuombe Musuguri kushikilia nafasi hiyo na kukiweka kijiji katika mstari kwa mwaka mmoja, ndipo ukafuatia uchaguzi.

Anasema, Musuguri hakutaka kugombea nafasi hiyo, ingawa wananchi walikuwa wanamhitaji awe kiongozi wake, lakini akakataa kwa maelezo kwamba mwaka mmoja alioongoza unatosha.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipomtembelea Jenerali Mstaafu David Musuguri, kijijini Butiama Mara.

Kwa muda huo, ameacha rekodi kuisaidia kufufua miradi ya kijiji ikiwamo duka la kijiji, mashamba, gereji, kiwanda cha mbao, pia akaimarisha umoja wa wananchi wa Butiama, uliokuwa umeyumba kutokana na kijiji kukosa uongozi kamili.

Anaongeza kuwa Musuguri alikuwa mtu wa karibu na wazee wenzake wa Butiama na alikuwa anashirikishwa katika mambo mbalimbali yakiwamo ya kimila ili kupata busara zake.

"Butiama wamepata pigo kubwa, kwani hapa tunapozungumza, watu wamefurika nyumbani kwake tangu wapate taarifa ya msiba, wanashinda hapo," anasema.

### AMGOMEA MTOTO WA AMIN

Maghembe anaisimulia Nipashe, kwamba Musuguri alikuwa mtu mwenye msimamo usioyumba, akitoa mfano tukio la mwaka 2008, kwamba mtoto wa Rais wa zamani wa Uganda Nduli Idd Amin alipotaka kuonana naye.

"Sikumbuki jina lake, lakini alikuwa ni mtoto wa kiume ambaye alikuja Butiama nyumbani kwa Baba wa Taifa akazungumza na familia, pia alitamani kukutana na Musuguri ili wazungumze," anasema.

Katibu huyo anasimulia Musuguri alikataa kuonana na mtoto wa Amin akisema "hawezi kukaa pamoja na mtoto wa mtu ambaye aliua Watanzania kwa uvamizi wake mkoani Kagera."

"Nilikuwapo wakati mtoto huyo anafika kwa Baba wa Taifa, sikujua alitaka kuzungumza nini, lakini Musuguri alikataa kuonana naye akisema hataki kuonana na mtoto wa mtu aliyeua Watanzania," anasema.

Anaeleza kwamba Musuguri hakuwa mtu wa kuyumba na kwamba msimamo huo ulimfanya mtoto wa Amin aliyekaa siku moja, aondoke Butiama bila kuonana na mkuu wa huyo wa majeshi mstaafu.

Jackton anasema hilo ni miongoni mwa matukio ambayo hatayasahau katika maisha yake kuhusu Musuguri, kwa maelezo kwamba alishuhudia hatua kwa hatua jinsi ambavyo mtoto huyo aliomba waonane.

### MTU WA WATU

Chifu Japhet Wanzagi, anamtaja Musuguri alikuwa mtu wa watu na mwadilifu, huku akifafanua kuwa nyumbani kwake kulikuwa kama 'kituo cha kulelea watu kutoka mikoa mbalimbali.

"Nyumbani kwa Musuguri kulikuwa kama kituo cha kulelea watu, kwani kila siku walikuwa wanajaa kumwelezea shida mbalimbali ili awasaidie, kwani hakukuwa na kizuizi cha kuonana naye," anasema Chifu Wanzagi.

Anasema sio kwamba alikuwa na fedha nyingi za kuwagawia, bali ni roho ya utu aliokuwa nayo na kwamba alijitahidi kuhangaika huku na kule kumsaidia kila mmoja kadri inavyowezekana.

Chifu Wanzagi anaongeza kusema kuwa Musuguri hakuwa tayari kuona mtu anakosa fedha za kusafirisha maiti kutoka maeneo mengine kwenda Butiama badala yake alijitahidi kuhakikisha anapata gari la kubeba maiti.

"Lakini pamoja na wema wake huo, baadhi ya watu walifikia kudanganya wakawa wanaomba kiasi fulani cha fedha kwa ajili kujitibu au kununua vifaa vya shule na kumbe si kweli," anasema.

Aidha, anasema Musuguri alikuwa anaishi nje kidogo ya mji wa Butiama, na kwamba watu walikuwa huru kufika nyumbani kwake kucheza bao, na hivyo kuufanya mji wake kufurika watu kila siku.

Kwenye suala la uadilifu, anasema Musuguri alikuwa mwadilifu kama Baba wa Taifa, akifafanua kuwa hakujilimbizia mali, bali aliishi katika nyumba za kawaida alizojenga kijijini Butiama.

Anasema amejengewa nyumba nzuri wakati wa utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano na kwamba hata hivyo hakuishi muda mrefu katika nyumba hiyo kutokana na kusafiri sana kwa ajili ya matibabu.

### AGAWIA MAJIRANI VIWANJA

Katika makazi yake mengine ya jijini Dar es Salaam, ambayo yapo eneo ambalo ni maarufu kwa jina la 'Kwa Musuguri', Kamanda huyo mstaafu aliwahi kugawa viwanja vyake bure kwa baadhi ya majirani.

Mkazi wa Mbezi Kwa Msuguri anayejitambulisha kwa jina la Leonard Mbangile, anasema Msuguri ana eneo kubwa ambalo baadhi ya watu walikuwa wameanza 'kujimegea' kinyemela.

"Familia yake ambayo inaishi eneo hilo, ilimpa taarifa, akaja kutoka Butiama na kukuta baadhi ya watu wamejenga vibanda ambavyo si vya kudumu," anasema Mbangile.

Anaeleza baada ya mbabe huyo wa vita ya Uganda kufika, aliamua kuwamegea watu hao sehemu ya kiwanja chake, huku akisema kuwa hao ndio majira zake ambao ataishi nao.

Anasema, alifanya tukio ambalo watu wengi walibaki wana shangaa, kwa kuwa walitarajia angewafukuza au kuwachukulia hatua za kisheria kwa kuvamia kiwanja chake, lakini akaonyesha uungwana.

"Mzee Msuguri alikuwa mnyenyekevu na msikivu, hatukukosea kumpa heshima ya kutumia jina lake kuliita eneo hili Kwa Msuguri tangu mwaka 1980 hadi leo limeendelea kuwa maarufu," anasema.

### SIRI YA MAISHA MAREFU

Msemaji wa Ukoo a Nyerere, anamwelezea, alikuwa ni mtu wa mazoezi, kwani alikuwa anatembea kila akitoka nyumbani kwake katika kitongoji cha Kitanga kwenda Senta au shambani.

Anaeleza alikuwa na mashamba, pia ng'ombe wengi wa kienyeji na kisasa, na alipendelea chakula cha kabila lake la Kizanaki ambacho ni ugali wa muhogo na mboga za majani, maziwa na nyama.

"Vilevile alikuwa anapenda kunywa uji wa ulevi, kwa mtindo huo wa maisha, ninaamini umechangia kumfanya aishi miaka mingi," anasema.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Majina ya watu mashuhuri yanapogeuka shubiri kwao






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

BAADA ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kutangazwa na Rais Benjamin Mkapa Oktoba 14, 1999 Ikulu ya Dar es Salaam, ndipo mawazo ya wengi yakakimbilia kwenye familia yake.

Watanzania wengi wakitaka kujua Mwalimu ameacha mjane na watoto wangapi na wako wapi na wanafanya nini. Tukaambiwa Mwalimu kaacha mjane, Mama Maria na wanawe wanane na wako nchini.

Tukatajiwa watoto hao wakifuatana kwa umri wao, kuwa ni Andrew, Anna (Watiku), Emil (Magige), John-Guido, Charles (Makongoro), Godfrey (Madaraka), Rosemary na Pauleta.

Wanane ni wa familia halali ya Mwalimu Nyerere.

Siku ya maziko yaliyofanyika Mwitongo, Butiama mkoani Mara, Oktoba 23, 1999 nilibahatika kuwapo na nikashuhudia wanawe hao wakiwapo, isipokuwa John, nilipouliza, nikaambiwa alikuwa ametoka kidogo.

Tulimaliza maziko wengine tukarudi mjini Musoma tulikokuwa tumepiga kambi baada ya kutoka Dar es Salaam, mahususi kwa ajili ya kumsindikiza mzee wetu huyo (77) aliyetoa mchango mkubwa kwa Taifa.

Tukiwa tumeshasahau msiba na kufanya mambo mengine, tukibakiwa na kumbukizi ya kila Oktoba 14 katika miaka ya kati ya 2000 likajitokeza jina jipya la familia ya Nyerere; Steve Nyerere.

Ikabidi nirudi kwenye makabrasha yangu na Halmashauri ya kichwa changu, kuona kama jina lile nililisahau wakati tunatajiwa familia ya Mwalimu au vipi! Nikajiridhisha kuwa hatukutajiwa idadi ya watoto tisa.

Niliendelea kutaka kujiridhisha, hata kutafuta kumwona Steve Nyerere ana kwa ana au hata kwa picha, nikafanikiwa kwa picha na sauti nikisikia akizungumza kama Mwalimu kabisa. Ilinipa shida kutoamini kama si mwanawe.

Maanake sauti ilinishawishi kuamini, ila umbile sasa! Katika familia ya Mwalimu Nyerere sikupata kumwona wa hivi na hata siku ya maziko hakuwapo!

Pengine alikuwa bado mdogo akawa amelala chumbani sisi tukizika! Yawezekana!

Ilibidi niulizie huku nikiendekeza ubishi niking'ang'ania sauti yake, kuwa asingeweza kuwa vile bila kuwa na vinasaba vya Mwalimu!

Nilipoendekeza ubishi waliokuwa wakinielimisha wakaniacha na ubozi wangu.

Hivi karibuni kwenye kumbukizi ya Mwalimu, nikamsikia Madaraka, mtoto wa Mwalimu, akimshauri Steve kuacha kutumia jina la Steve Nyerere moja kwa moja bali aenzi wazazi wake.

"Kabla ya kuenzi viongozi, tuanze kuenzi wazazi wetu..." akashauri Madaraka huku akishangaa eti Steve ameona haitoshi yeye kujiita Steve Nyerere, akisikika kampa mwanawe jina hilo na sasa anaitwa Alex Nyerere!

Nikajiuliza baya ni lipi hapo, mbona Nyerere na Mengele yote yana herufi saba? Pengine ndicho kigezo alichotumia.

Lakini, nikauliza asili ya Steve, nikaambiwa ni mkoa fulani, huku Madaraka akizidi kusigina kuwa katika ukoo wao pia kuna Steve Nyerere, lakini si msanii.

Akaniacha hoi, alipohoji kama Steve Nyerere wa huko mbali atahudhuria vikao vya familia ya Mwalimu, ambavyo hufanyika kila miaka miwili Mwitongo. Kazi itakuwa kwa Steve wa maigizo kama atahudhuria au la.

Steve mwenyewe huko alikokuwa aliposikia malalamiko ya Madaraka, akaweka mguu chini... ingawa ushauri wa Madaraka ni kwamba aitwe Steve Mengele aka Steve Nyerere na si kulitwaa kiujumla jumla kana kwamba alipewa na wazazi wake.

Kuna msomi fulani yeye akaja na hoja kuwa ni vema wasanii wakang'ang'ania majina maarufu, ili waendelee kupata ugali wao kupitia majina hayo.

Angoje sasa watu waje na hatimiliki za majina ndipo wataonja joto ya jiwe. Utumie jina langu kula nikuache! Thubutu!

Kwanini Steve asikubali tu yaishe? Kwani kwao Nyerere linamaanisha nini? Kwa sababu majina yana asili na maana, hayashuki hivi hivi kama mvua! Ndiyo maana Wazanaki wana maana yake.

Hoja ya Madaraka imenipa funzo kuwa kuenzi wazazi ni jambo la msingi sana, hasa kwa nyie mnaoweka picha za watu mashuhuri na hasa viongozi na matajiri kwenye 'profiles' za simu zenu!

Mnaacha zenu na za wazazi na ndugu zenu, mnakumbatia watu baki kwa ukwasi na madaraka yao.

Pia, ninyi mnaojipachika majina ya Wazungu na kuacha ya asili yenu kwa kutafuta hulua, hasa mnaojiita wanamuziki na wasanii, kwani ukitumia jina lako kazi yako haifanikiwi?

Kama unaitwa Mgagagigikoko na unaimba vizuri kuna shida? Unaitwa Shokolokobangoshey unacheza vizuri kuna tatizo? Acheni hizo!

BIASHARA

MIGONGANO WANYAMA NA WANADAMU...

# Wajerumani na wana - Namtumbo walipoingia ubia kumaliza kasoro

**Na Jenifer Gilla**

LICHA ya utalii wa wanyamapori kuwa sekta iliyo juu kuingizia taifa mapato, kutokana na fedha za kigeni, inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Sasa imefika hatua inaleta madhara kwa binadamu, ikiwamo kuharibiwa vyanzo vya mapato kama vile mashamba na vyakula na kuwaacha wakiwa katika hali ya umasikini kwa muda mrefu.

Kwa upande wa pili, wanyamapori pia huathirika, kwa sababu binadamu hulipiza kisasi kwa kuwadhuru kutokana na uharibifu wanaofanyiwa.

Kitakwimu, Sekta ya Maliasili na Utalii, inachangia pato la taifa kwa asilimia 17.5 na fedha za kigeni asilimia 25, pamoja na kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja Mil. 1.5.

Hata hivyo, Sekta ya Utalii na Wanyamapori inakabiliwa na changamoto mbalimbali, kubwa ikiwa migogoro na binadamu inayosababisha madhara kwa pande zote mbili.

Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2012 hadi 2019, watu 642 wamejeruhiwa, pia 1069 wamepoteza maisha na mifugo 792 iliuawa; vilevile kuna ekari 41,041 za mazao zimeharibiwa, kutokana na migongano hiyo baina ya binadamu na wanyamapori.



Wanakijiji Kitanda, wakisafisha mahindi yaliyouzwa na wakulima katika Kituo cha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, kijijini hapo. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA**

### KUTOKA NAMTUMBO

Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, ni moja ya maeneo yanayotajwa kukabiliwa na changamoto ya migongano kati ya binadamu na wanyamapori.

Hiyo ikasababisha uharibifu mkubwa wa mazao na kuwaacha wanakijiji katika umaskini, huku wakilipa kisasi kwa kuwawinda na kuwaua wanyama hao.

Kwa kutambua umuhimu wa binadamu na wanyamapori kuishi pamoja na kutegemeana, Halmashauri ya Namtumbo kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), wamebuni mikakati ya kupunguza kuelekea kabisa migogoro hiyo.

Taasisi hizo zilikaa pamoja na kuibua miradi ya miradi ya kibunifu, inayohakikisha kuwa makundi hayo yanakaa pamoja kufurahia rasilimali zinazowazunguka. Mbinu hizo ni kama vile elimu kwa jamii namna ya kukabiliana na wanayamapori waharibifu na kuwafundisha fursa zinazopatikana kutokana na uwapo wa wanyama hao, ili wawaone sehemu ya maendeleo na si maadui.

Mshauri wa Kiufundi wa GIZ - Namtumbo, Chrian Zimbai, anawaambia waandishi wa habari, Chama cha Wanahabari wa Mazingira Tanzania (JET), anasema GIZ inaiongezea nguvu halmashauri hiyo kupunguza migogoro ya watu na wanyama.

Chrian anasema, katika wilaya hiyo wanatekeleza mradi wa miaka mitatu ulioanza 2022 ukilenga kumaliza migongano kati ya binadamu na wanyamapori, wakishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii katika vijiji vya Mtelawamwahi, Ligunga, Kilimasera, Mtonya na Kitanda.

Anasema kupitia mradi huo wanaijengea uwezo Halmashauri ya Namtumbo, namna ya kukabiliana na wanyama waharibifu, wanaipa ruzuku iwasaidie kuweka mafuta kwenye magari na kuwapa posho askari wa wanyamapori wa vijiji ili kuwarahisishia wanapokwenda kutekeleza majukumu ya uhifadhi.

Ofisa huyo anaeleza kwamba, pia wanawapa vitenda kazi vya utekelezaji shughuli hizo ikiwamo pikipiki, kompyuta na vinavyohitajika kufukuza tembo kama vile dawa zenye harufu kali.



Chrian Zimbaiya, Mshauri wa Kiufundi wa Taasisi ya GIZ, Namtumbo, Ruvuma.

Anasema kutokana na bajeti ndogo ya wilaya iliyotengwa kwa ajili ya kupunguza HWC, taasisi hiyo ya GIZ iliamua kutoa ruzuku ya shilingi milioni 120 kusaidia mafuta, sare, posho na hema. Vilevile wanatoa mafunzo ya kuweka vizuizi. Hiyo ni kama vile fensi yenye pilipili ili kuzuia wanyamapori waharibifu kama vile tembo kuingia katika makazi ya au maeneo ya kilimo, na hivyo kupunguza matukio ya migogoro.

"Ama kwa kuhamasisha matumizi endelevu ya ardhi au kwa kuhimiza mbinu za matumizi ya ardhi zinazooana na makazi ya wanyamapori, tunaweza kusaidia kupunguza migogoro kwa kuunda maeneo ya 'buffer' au korridoni za wanyamapori," anasema.

Anasema, pia wanatoa mafunzo kwa jamii juu ya tabia za wanyamapori watambue namna ya kuishi nao na kujiepusha na uharibifu ikiwa ni mbinu mojawapo kuboresha uwezo wao wa kupunguza migogoro kwa amani.

Lingine anasema, wanasaidia kwa zana za mafunzo ya Askari wa Wanyamapori wa Vijiji (VGS) katika Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Jamii, kilichoko Likuyu Sekamaganga, kuwafundisha jinsi ya kushughulikia wanyamapori wakorofi na waharibifu.

Mradi huo anasema wanautekeleza katika Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi na wilaya za Tunduru mkoani Ruvuma.

Mhifadhi wa Wanyamapori wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Issa Ndomondo, anasema, wamekuwa wakiwashauri wanakijiji kutumia mbinu zilizotolewa na wataalamu kufukuza wanyamapori, mbinu sasa zinajulikana, hazina zenye ufanisi mkubwa.

"Changamoto ilikuwa kubwa zaidi kabla ya GIZ kufika wilayani kwetu," anasema, akibainisha kuwa watu wanashukuru kwamba matukio ya tembo kuvamia mashamba yamepungua katika vijiji vingi.

"Changamoto za HWC zimepungua katika vijiji vitano vilivyohusika kwenye mradi. Ni vijiji vitatu pekee bado vilikabiliwa na tatizo," anasema kama GIZ isingechukua hatua hiyo, uharibifu wa mazao katika vijiji hivyo, hasa Likuyu Sekamaganga, ungekuwa mkubwa zaidi.

### SABABU MIGOGORO

Ndomondo anataja sababu zinazochochea migogoro hiyo, ni ongezeko la makazi na idadi kubwa ya watu, zinazosababisha ardhi kuwa finyu na kushawishi wanakijiji kwenda kufanya shughuli za kiuchumi, kama vile kilimo kwenye mapito ya shoroba.

Anataja sababu nyingine, ni uingizaji mifugo katika maeneo ya hifadhi, mabadiliko ya hali ya hewa yanayoleta ukame na njaa kwa wanyama, hivyo wanavamia maboma kusaka mahitaji yao.

Katibu wa Kimbanda, Jumuiya ya Wanyamapori ya Kimbanda (WMA), Juma Kihindo, kwa kushirikiana na GIZ, wakaanzisha miradi ya usimamizi endelevu wa misitu, ikiwamo ya kuuza hewa ya safi inayosaidia kunyonya hewa chafu ya kaboni.

Hiyo, ndio ikawawezesha wakazi wa maeneo yanayozunguka kama vile Lusewa, Milonji, Ligunga, Matepwende, Msisima, Mnalawi na Malalawima kunufaika kiuchumi.

Anasema kabla ya miradi huo - Kimbanda WMA, ilikabiliwa na mwingiliano na wanyamapori, ikawafanya binadamu kuwawinda na kuwadhuru wanyama hao, kwa dhana "si rafiki kwa maisha yao."

"Kimbanda WMA tayari imeingia makubaliano na Carbon Tanzania (kampuni). Ushirikiano huu ni hatua kubwa kuelekea jitihada za uhifadhi endelevu na uangalizi wa mazingira katika eneo hili," anasema.





# Mamlaka za maji zatakiwa kutoa taarifa sahihi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA za Maji na Usafi wa Mazingira nchini zimetakiwa kutoa taarifa sahihi kuhusu uendeshaji na utoaji wa huduma ili zitumike katika utekelezaji wa mipango ya serikali na kuimarisha sekta ya maji nchini.

Maelekezo hayo yalitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Dk. James Andilile, wakati akifungua kikao kazi cha kuhakiki taarifa kwa watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Wilaya na Miji Midogo.

Dk. Andilile alisema kuwa, EWURA imetathmini taarifa zote zilizowasilishwa na mamlaka hizo katika mfumo wa Majls kwa mwaka 2023/24 na kubaini takwimu zisizo sahihi za kiwango cha maji yanayozalishwa, muda wa upatikanaji wa huduma, usimamizi wa usafi wa mazingira, hali ya upatikanaji na kiwango cha uhitaji wa maji, ubora wa maji na upotevu wa maji.

**"Kazi yetu kubwa ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora ya maji na inayokidhi mahitaji yao ya kila siku, tunapokosa takwimu sahihi,...**

"Kazi yetu kubwa ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora ya maji na inayokidhi mahitaji yao ya kila siku, tunapokosa ....takwimu sahihi, ni ngumu kuwapatia wananchi huduma hiyo, hivyo mnatakiwa mtoe kipaumbele katika kuwasilisha takwimu na ziwe sahihi," alisema.

Naye Mhandisi Jovitus Kichum, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, aliwasisitiza watendaji hao kuhakikisha takwimu zinazowekwa kwenye mfumo wa MajIs zinaakisi uhalisia ili serikali iweze kutatua changamoto zinazojitokeza kwa lengo la kuimarisha huduma za majisafi na usafi wa mazingira nchini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisalimiana na wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi ya Mother of Mercy ya jijini Dodoma kwenye viwanja vya Bunge, jana. **PICHA: OWM**

# 'Tumieni mwongozo kufahamu vyakula kuimarisha lishe'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kutumia mwongozo wa chakula na ulaji uliozinduliwa na serikali ili kufahamu vyakula gani na kwa kiasi gani wanapaswa kula kila siku ili kuimarisha lishe na kuacha kutumia 'Google' kama sehemu ya kupata utaratibu wa milo bora.

Ofisa Lishe kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Stella Kimambo, alisema hayo jana wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu siku ya lishe kitaifa ambayo huadhimishwa Oktoba 30 kila mwaka.

Kimambo alisema mwongozo huo wa chakula na ulaji ulizinduliwa Novemba 2024, ambao unaeleza vyakula ambavyo watu wanapaswa kula kila siku ili kuimarisha afya zao na kuondokana na magonjwa mbalimbali ikiwamo yasiyo ya kuambukiza.

"Mwongozo huu ulizinduliwa mwaka jana na serikali hivyo watu wanapaswa kuzingatia maelezo yaliyoko katika mwongozo huo ili kula vyakula ambavyo vitasaidia kulinda afya zao kwani umegusa makundi ya lika zote watoto hadi wazee.

"Badala ya watu kutumia Google kama sehemu ya kufahamu nini wanapaswa kula, hiyo siyo sahihi kwani ulaji wa vyakula unatofautiana kulingana na mazingira, hata chungwa linalolimwa Tanzania sio sawa na lile la nchi nyingine," alisema.

Aidha, alisema matumizi ya mwongozo huo yatakuwa msaada zaidi kwa Watanzania badala ya matumizi ya Google na kwamba ipo haja kwa jamii kuusoma na kutumia ili kuwa na kizazi chenye lishe bora.

Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Lishe Wizara ya Afya, Neema Mwapili, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya lishe nchini wanaendelea kushirikiana kuusambaza mwongozo huo ili kumfikia kila mtu.

Vile vile, alisema ili kuwa na jamii yenye lishe bora serikali imeendelea kuboresha afua mbalimbali za masuala hayo nchini.

Kadhalika, alitoa rai kwa shule zinazotoa chakula kwa wanafunzi kuhakikisha kuwa kinakidhi maelekezo ya serikali ili kiwe na tija kwa wanaokitumia.

"Chakula kinachotolewa shuleni lazima kiwe mchanganyiko sio kila siku wali maharage, lakini pia lazima vyakula viongozwe virutubishi kama ni unga wa mahindi ama wa ngano lazima uwe na virutubishi, lakini pia kwenye chumvi lazima kuwapo na madini joto," alisema Mwapili.

# Waandishi wapewa somo kuelekea uchaguzi S/Mitaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KUELEKEA uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu 2025, Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), umewataka wanahabari kutimiza wajibu wao wa kuandika habari zitakazowasaidia wananchi kufanya maamuzi sahihi.

Rais wa UTPC, Deogratius Nsokolo, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Singida kuhusu mkutano mkuu wa mwaka wa UTPC unaofanyika mkoani Singida kuanza leo Novemba mosi.

"Uchaguzi ni zoezi moja kubwa sana kwani kupitia viongozi ndipo unaweza kupata kiongozi bora au wa ovyo, hivyo basi wanahabari tunapaswa kutimiza wajibu wetu wa kuwafanya wananchi waweze kuchagua viongozi bora ambao watakuja kusaidia maendeleo yao," alisema.

Nsokolo alisema UTPC inawajibika kutoa mafunzo kwa wanahabari kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaofanyika mwaka huu uchaguzi mkuu mwakani ili kuwajengea uwezo waandishi wa habari waweze kusaidia wananchi kuchaguzi viongozi wazuri.

"UTPC ambayo inaongoza klabu 28 za waandishi wa habari Tanzania Bara na Visiwani na inahudumia takribani waandishi 2000 kwa vyovyote jambo ambalo linahusiana na uchaguzi ni jambo kubwa sana ambalo linakwenda kuleta viongozi kwenye taifa letu ambao watakuja kusimamia maendeleo ya nchi hii," alisema.

Akizungumzia mkutano mkuu wa UTPC, akisema utafunguliwa leo (Novemba mosi, 2024) na Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda na utahusisha wajumbe watatu kutoka kila mkoa ambao ni Mwenyekiti wa Klabu, Katibu na Mweka Hazina.

Alisema Novemba 2, UTPC itatoa tuzo za weledi kwa waandishi wa habari ambao wameandika habari zilizoleta matokeo chanya katika jamii na zitatolewa na Mkuu wa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego.

Mkurugenzi Mtendaji wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Kenneth Simbaya, alisema suala la kuwajengea waandishi uwezo au ujuzi wa kuandika habari za uchaguzi zenye weledi limepewa kipaumbele na UTPC.

"Tunapompa mwananchi habari ndipo wanaweza kuchagua viongozi sahihi, hivyo kama taasisi tunalipa kipaumbele kikubwa suala la kuwapa mafunzo waandishi kwani tunaamini endapo waandishi hawatawapa wananchi habari sahihi hawatachagua viongozi ambao ni sahihi wa kuwaletea maendeleo," alisema.



# Viongozi wajipambanua kampeni, uchaguzi mitaa

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe kimesema kitafuata sheria na miongozo ya wasimamizi na kutoruhusu lugha za matusi na zisizo za staha wakati wa kampeni za uchaguzi wa wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji mwezi ujao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa CCM wa mkoa huo, Deo Sanga, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

"Sisi Chama Cha Mapinduzi ni chama kikubwa sana, ni chama ambacho kinaheshimu sana misingi ya kanuni ya Tume ya Uchaguzi kwa hiyo kanuni zile zinatupelekea tuwe na staha ya maneno ya kusema, tusiwe na maneno ambayo yanamwathiri mtu mwingine," alisema Sanga.

Aliwapongeza wanachama wa chama hicho waliojitokeza kugombea nafasi mbalimbali na wengine kushiriki kupiga kura za maoni ndani ya chama hicho.

**"Lengo letu CHADEMA ni kuhakikisha tunashinda uchaguzi wa serikali za mitaa kwa asilimia 95, hatupendi tushinde mitaa yote kwa kuwa tutakosa watu wa kutukosoa na tutafanya**

Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Jimbo la Makambako, Daudi Tweve alisema chama hicho kimejipanga kushiriki uchaguzi kwa kusimamisha wagombea kila mtaa, kijiji na kitongoji. "Lengo letu CHADEMA ni kuhakikisha tunashinda uchaguzi wa serikali za mitaa kwa asilimia 95, hatupendi tushinde mitaa yote kwa kuwa tutakosa watu wa kutukosoa na tutafanya vibaya," alisema Tweve.

Alisema CHADEMA hawaamini katika utawala wa chama kimoja kwa sababu uongoze vizuri na uzingatie utawala bora unahitaji uwe na watu ambao watakosoa pale unapokosea.

Katibu Mwenezi wa ACT Wazalendo mkoani hapa, Ally Mhagama, alisema chama hicho kinaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili washiriki uchaguzi na kutoa rai kwa wanasiasa pindi kampeni zitakapoanza kuacha kutumia lugha chafu na kushindana kwa hoja.



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke, Abdallah Mtinika (mwenye suti), akifurahia jambo na vijana wa bodaboda, baada ya kupata mkopo kutoka Benki ya Biashara ya DCB, katika hafla iliyofanyika Mbagala, Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kijana matatani kwa kujaza magunia ya mahindi mchanga

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamshikilia Mkazi wa Kijiji cha Palangawanu Wilaya ya Wanging'ombe (31) kwa tuhuma za kujaza magunia 115 mchanga kwenye ghala la kuhifadhia mahindi kwa lengo kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alisema kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa Oktoba 23, mwaka huu kijijini hapo.

Banga alisema kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa kwa tuhuma hizo baada ya kupewa kazi ya kusimamia ghala hilo ambalo lilikuwa na magunia ya mahindi 2,063, kila moja lilikuwa na wastani wa madebe tano.

"Kila debe lilikuwa linauzwa kwa shilingi 10,000 na baada ya upekuzi imebainika kumekutwa magunia 610, magunia ya mchanga 115 tofauti na magunia yaliyobakia yameuzwa na kijana huyu na tunamshikilia kwa tuhuma hizo," alisema kamanda huyo.

Alisema kutokana na kuaminiwa kwa mtuhumiwa huyo, wakulima wengine walimpatia madebe 6,335 ya mahindi yenye thamani ya zaidi shilingi milioni 63 kwa mali kauli.

"Alipokwenda kuziuza kwa maelezo yake jijini Dar es Salaam fedha hizo bado hajarejeshewa ndio sababu ya wakulima kudai mahindi katika kijiji hicho," alisema.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, upelelezi ukikamilika, mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

Banga alitoa wito kwa wafanyabiashara kuacha tabia za kujaza mchanga katika magunia na kuwaibia wakulima kwa sababu vyombo vya dola vipo macho na vitachukua hatua kwa mujibu wa sheria.

Mmoja wa wakulima hao, Dickson Makoga alisema mtuhumiwa huyo alikuwa akipita na kupima mahindi na kuyahifadhi katika ghala hilo kwa makubaliano ya kuwalipa fedha baada ya kuyauza, atatukabidhi fedha lakini hakufanya hivyo.

# Wanaume wadaiwa kuchangia udumavu watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BAADHI ya wanawake wa Kata ya Maguvani Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani hapa Mkoa wa Njombe wamedai waume zao chanzo cha udumavu kwa kuwaachia jukumu la kuwahudumia watoto na kukosa lishe bora.

Vilevile, walidai kipato duni na kukosa elimu ya uandaji chakula bora kwa kuzingatia makundi sita ya vyakula ni sababu nyingine inayochangia udumavu mkoani Njombe licha ya kuwa na mazao ya nafaka, mbogamboga na matunda

Madai hayo waliyatoa juzi wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Lishe yaliyofanyika Soko la Maguvani mjini Makambako.

Wanawake hao, akiwemo Nazalena Kivike, alidai kutokana wengi wao kutumia muda mwingi kwa shughuli za uchumi wanakosa muda wa kunyonyesha watoto kwa wakati na kuwaandalia chakula, hivyo kupata udumavu.

"Majukumu ya familia katika malezi tumeachiwa sisi, inatulazimu kulea familia na kutafuta fedha," alisema Nuru Mkufi.

Ofisa Lishe wa Halmashauri hiyo, Christina Mwazembe, aliwataka wananchi kuzingatia makundi hayo sita ya chakula ili kukabiliana na udumavu na kuongeza mahudhurio ya wanafunzi shuleni.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri iyo, Masinde Masinde, alisema udamavu umesababisha watu kuwa tegemezi na kusubiri wazazi kufa ili warithi mali.

"Na hivi vitendo vya ubakaji na ulawiti kwa watoto na wanawake pia huu ni udumavu, inakuwaje babu mwenye miaka 65 anaenda kubaka mtoto wenye miaka 10, kama siyo udumavu ni nini?" Alihoji.

"Udumavu unaathiri jamii kwa kiasi kikubwa sana, wengi wanashindwa kufanya maamuzi sahihi na yenye tija kutokana na ubongo kutofanya kazi kwa ufanisi," aliongeza kusema Masinde.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Alexander Mchome, aliwataka wananchi kutambua udumavu kwa watoto unaanzia ndani ya siku 1,000 toka mama anapopata ujauzito kwa mara ya kwanza na kuwahimiza wanaume kushiriki kwenye malezi ili kukabiliana na tatizo hilo.

Diwani wa Kata ya Maguvani na Mwenyekiti wa Halmashauri ya mji wa Makambako, Hanana Mfikwa, aliwataka wananchi kuzingatia elimu inayotolewa ili kukabiliana na magonjwa yanayosababishwa na kukosa lishe bora.

Kauli mbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni "Mchongo ni afya yako, zingatia unachokula."



# Norway kufanya utafiti afya ya udongo Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, imepokea ujumbe wa taasisi ya utafiti wa kilimo kutoka nchini Norway kwa lengo la kufanya utafiti wa afya ya udongo ili kukuza uzalishaji wa mazao ya chakula visiwani humo.

Akizungunza jana na ujumbe huo, Wizara ya Kilimo Maruhubi mjini hapa, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ali Khamis Juma, alisema kufanyika kwa utafiti huo ni kupata fursa kuongezeka kwa mazao ya chakula.

Alisema utafiti huo utaonesha jinsi Zanzibar inavyokuwa bora katika miundombinu ya kilimo kwa vile wananchi wake wengi wanajishughulisha na sekta hiyo kwa ajili ya chakula na biashara.

Alisema hali halisi ya ardhi ya Zanzibar ni ndogo na idadi ya watu inaongezeka, kuwapo kwa utafiti huo kunawafanya wakulima kulima kilimo bora na kutumia ardhi ndogo na kupata mazao mengi tofauti na ilivyo sasa.

"Ardhi ya Zanzibar kiuhalisia ni ndogo na kila kukicha watu wanaongezeka, lakini jambo la kufurahi utafiti huo sasa utawafanya wakulima wa Zanzibar kutumia ardhi ndogo, lakini mazao ya wakulima yatakuwa mengi," alisema.

Aidha, alisema Serikali ya Zanzibar ipo mstari wa mbele kuzungumza na wadau wake ili wakulima wanufaike ikiwamo kupata mazao ya kwa ajili ya chakula na biashara.

Alisema taasisi ya utafiti ya Norway kuja na kufanya utafiti wao visiwani humo kutawapa nafasi wakulima kulima kilimo cha biashara kwa muda wote na kuifanya Zanzibar kuendelea kuwa na uhakika wa chakula muda wote.

Alisema ujio huo kufika Zanzibar unatokana na ziara ya Rais Samia Suluhu kuitaka nchi ya Norway kupitia taasisi hiyo kufika Tanzania kushirikiana katika utafiti.

Alisema, licha ya Tanzania Bara kuanza utafiti huo kwa miaka mitatu, lakini bado wataendelea kushirikiana nao ili kuona malengo yanafikiwa kwa pande zote mbili.

**Alisema, licha ya Tanzania Bara kuanza utafiti huo kwa miaka mitatu, lakini bado wataendelea kushirikiana nao ili kuona malengo yanafikiwa kwa pande zote mbili.**

Naye Profesa Udaya Sekher Nagothu kutoka taasisi hiyo alisema kuwa nchi ya Norway ina ushirikiano mkubwa wa kimaendeleo na Tanzania ikiwamo Zanzibar na kufanyika kwa utafiti huo kunaenda kuongeza ushirikiano mwingine wa kitaaluma.

Alisema wameamua kuja Tanzania na kufanya utafiti huo kutokana na Rais Samia kuwaomba kushirikiana katika kazi ya utafiti wa afya ya udongo ili kukuza mazao na kuondoa changamoto katika udongo.

"Ujumbe wetu huu ni wa umuhimu mkubwa kwa vile Rais Samia alituomba kushirikiana na Tanzania ikiwamo Zanzibar katika suala la utafiti wa afya ya udongo ili kukuza mazao na sisi tuko tayari kwa hili," alisema profesa Udaya.

Mkurugenzi Mkuu wa utafiti wa kilimo Tanzania, Dk. Thomas Bwana, alisema kumeshaanza kufanyika utafiti wa udongo kwa kipindi cha miaka mitatu ili kukuza kilimo kuwa bora.

Alisema kuwa jambo la kujivunia kwa kipindi hicho tayari wanavituo 17 vikubwa na 18 vidogo na wakulima wameshaonesha nia ya utayari wao ili kulima kilimo chenye tija na kupata masoko mazuri.

"Kwa kweli bado hatujaonesha nia juu ya zao gani litalopewa kipaumbele katika utafiti huo, lakini wakulima wako tayari kulima kilimo chenye tija na kupata masoko," alisema Thomas.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Dk. Mohamed Dhamir Kombo, alisema kufanyika kwa utafiti huo Zanzibar kutaongeza fursa kwa wakulima na Zanzibar ambayo ina wakulima wengi, lakini changamoto ni masoko.

Aidha, alisema ZARI imefanya utafiti mbali mbali wa kilimo ikiwamo utafiti 200 Pemba na 300 kwa Unguja na kubaini mambo mengi ikiwamo baadhi ya ardhi kukosa madini chuma. Utafiti utakaofanywa na Norway utatoa jibu sahihi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akiweka mchanga kaburini wakati wa maziko ya aliyekuwa Ofisa Utumishi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba, marehemu Ali Massoud Ali, aliyezikwa kijijini kwao, Uvumbi, Wilaya ya Chakechake, Pemba, jana. **PICHA: OMPR**

## Jamii yahamasishwa matumizi ya nishati safi ya kupikia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Viti Maalumu Mkoa wa Kaskazini Unguja Riziki Pembe Juma, ameitaka jamii kuachana na matumizi ya kuni na mkaa na badala yake watumie nishati safi ya gesi ili kurahisisha harakati zao.

Pembe ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, aliyasema hayo katika mkutano wa wajasiriamali wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, katika ugawaji wa majiko ya gesi hafla iliyofanyika katika Ofisi ya Mkoa Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia jamii kuwa na afya bora kwa kuepukana na madhara ya moshi unaotokana na matumizi ya kuni pamoja na kupika kwa uharaka zaidi.

Aidha, aliwataka wanawake wa mkoa huo kujiunga na vikundi ili kuwarahisishia kupata fursa za mikopo kwa haraka ili kujikwamua kiuchumi na kukuza biashara zao.

Waziri Pembe, aliwataka wajasiriamali hao kutojirahisisha katika biashara zao kwasababu inaweza kuchochea vitendo vya udhalilishaji na pia kuwa makini katika kuwafuatilia watoto wao huku wakiendelea na biashara zao, kwa kujua mienendo yao ili kuwakinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi yao.

Wakitoa maoni yao baadhi ya wajasiriamali hao, waliishukuru serikali kwa kuamua kumtua mama kuni kichwani na kuwasaidia kupata majiko hayo ambapo pia wameiomba serikali kuwapatia vifaa vya kazi zao ili kujikwamua zaidi kimaisha.

Ugawaji wa majiko ya gesi hayo kwa kinamama ni kampeni maalumu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha inamtua mama kuni na kutumia nishati safi ya kupikia.

# UWT yawafunda wanawake jukumu la utendaji

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Wanawake CCM (UWT) Mkoa wa Kaskazini Unguja umesema jukumu la utendaji wa pamoja na uchapakazi, bidii, maarifa na uzoefu ni dira ya kufikia malengo ya kukuza haiba ya maendeleo ya siasa.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kaskazini Unguja, Maryam Muharrami Shomari, alisema hayo Mahonda mkoani humo wakati akimkaribisha Katibu mpya wa umoja huo mkoani humo, Rehema Kondo Kombo.

Maryam alisema utendaji wa kazi za UWT uwaunganishe wanachama wake wote ili kukisaidia chama chao na kukipatia ushindi CCM ili kishike dola.

"Tunakukaribisha katibu Mkoa Kaskazini. Karibu usimamia kanuni ya UWT na katiba ya CCM. Tunategemea uwe kiungo kwa jumuiya. Utendaji kazi wa pamoja utatuletea mafanikio na maendeleo yatakatotupa heshima," alisema Maryam.

Alidai, hakuna nyumba hata moja duniani, iliyojengwa na fundi mmoja ikamalizika na kupendeza, badala yake hujengwa kwa ushirikiano na mafundi aina tofauti wa ujuzi na ufundi usiofanana.

"Wapo mafundi ujenzi, umeme, maji na waweka bati. Wapo wajuzi wa kutia marumaru na nakshi. UWT ina kazi ya kuhakikisha serikali mbili zinaendelea kuungwa mkono na wananchi," alisema.

Hata hivyo, alisema hakuna sababu hata moja itakayowafanya wanawake, washindwe kufikia malengo ya UWT ikiwa watafuata na kuheshimu kanuni, kuishi kimaadili na utii wa Katiba ya CCM.

Pia, alisema kila zikitokea tofauti za kibinadamu, viongozi wajenge uvumilivu, subira na kuzungumza chini kwa kufuata falsa ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan.

"R4 ni formula ndani ya dola, kwenye taasisi za kiserikali, zisizo za kiserikali, kijamii na kisiasa. Dhana ya uvumilivu, umakini, uwajibikaji na uwazi ni mambo yanayohitajika," alisema.

Naye Katibu mpya UWT Mkoa Kaskazini Unguja, Rehema Kombo, alisema atazingatia ushauri wa Mwenyekiti wa mkoa na kuahidi kusimamia kanuni ya UWT na kuchapakazi bila hofu.

Alisema kazi ya kuendeleza UWT si ya mtu mmoja na kwamba kila mwanachama kwa umuhimu na wakati unaostahili, ajitolee kadri ya uwezo wake kufikia malengo kwa hekima, juhudi na ufanisi.

## TANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**PLASIDI FRANCIS MASSAWE** anatangaza kupotelewa na cheti. Namba ya mtihani **NS1513/0063/2017.** Aina ya mtihani **CSEE.** Mwaka wa mtihani 2017. Jina la shule **SOMSOM SECONDARY.** Mahali cheti kilipo potelea **KIBAHA MAILIMOJA.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi: Control No. **9910842631062.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SIMON VARISANGA MODEST** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index namba **S5290/0114** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **CHRISTON SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021, cheti hiki kimepotea Mkoani Dar es salaam. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/234706/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**LINDA THOBIAS NGENDABANYIKWA**

Anatangaza kupotelewa na kadi za gari zenye namba za usajili **T126 DRZ, T347 DQV, T354 DCX, T616 AGW, T801 BLW.** Kwa yeyote atakaezioна atoe taarifa kituo cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/11845/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 170 & 171 YA 2024**

**STELLA PATRICK PASILIKA....................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **SALIMU OMARY SEMBE**
2. **HUSSEIN SENNI PULI**
3. **BINURU RAJABU SEMBE**
4. **ZAINABU RAMADHANI**
5. **LONGIDO AUCTION.........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**BINURU RAJABU SEMBE**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 26/11/2024 mbele ya Mwenyekiti E. MOGASA wewe mwenyewe au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 26 mwezi Novermber, 2024.

E. MOGASA
MWENYEKITI.
31/10/2024

**IN THE DISTRICT COURT OF IRINGA**
**AT IRINGA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26519 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DAVIS LEWIS POYO**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**MORRIS MCHINDIUZA POYO AND**
**RICHARD WILLIAM MCHINDIUZA**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22nd day of NOVEMBER 2024.
The Will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court.
Date at 31st this October day of 2024.

..............................................
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
IRINGA

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KILOSA**

**KITUO CHA MIKUMI MKOA MOROGORO**

**SHAURI LA MADAI/NDOA NA 87/2024**

**JINA LA MDAI: ANTHONY MWAIKENDA MWALUSAMBA**

**JINA LA MDAIWA: ADREW TUNGARAZA**
**KUITWA SHAURIN MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa:ANDREW TUNGARAZA**

**POPOTE ALIPO-TANZANIA,USIPOFIKA TAREHE HIYO SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA kwakuwa Mdai/Mdaiwa ameleta /wameleta Madai yake/yao kwamba(eleza hapa habari za mdai) MADAI YA FEDHA TSHS 5,185,000/=**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafisi katika Mahakama hii tarehe 19 mwezi wa 11 mwaka2024 saa5:00asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shauri ,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 Mwezi10 Mwaka 2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 30 YA 2024**

**WINIFRIDA WILLIAM WILLIAM.........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **AUBI MTASIWA**
2. **NATHANIEL ADAM KICHULUMBI......MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**GROLIA KALINGA(THIRD PARTY)**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 25/11/2024 mbele ya Mwenyekiti E. MOGASA wewe mwenyewe au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hutahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 23 mwezi Oktoba, 2024.

E.MOGASA
MWENYEKITI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MADAI No. 36/2024**

**MDAI............................SWAIBU JOSEPH**

**MDAIWA.....JAHANES JOHNBOSCO KANYOMOZA**

**KUITWA SHAURINI**

**Ndugu JOHANES JOHNBOSCO KANYOMOZA – POPOTE PALE ULIPO**

Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria tarehe 13-11-2024 bila kukosa.
Kama hutohudhuria basi shauri hili litasikilizwa upande mmoja wa uamuzi utatolewa.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO BUGENE
RESIDENT MAGISTRATE
PRIMARY COURT
KARAGWE

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MBEYA**
**LILILOPO MBEYA**
**MAOMBI MADOGO NA.106 YA MWAKA 2014**
**ELIUD MBALA::::::::::::::::::::::::::::::::MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1.WESTON SIMWELU:::::::::::::::::::::MJIBU MAOMBI**
**2.ABDALAH PATRICK MAFWANGA::MJIBU MAOMBI**
**3.THOMASI SIMON HALINGA::::::::::MJIBU MAOMBI**
**4.MUSSA LUVANDA::::::::::::::::::::::::MJIBU MAOMBI**
**5.JOYCE MWASHIUYA::::::::::::::::::::MJIBU MAOMBI**
**6.BENARD MWAMPAMBA::::::::::::::MJIBU MAOMBI**
**7.TUMA KABASA:::::::::::::::::::::::::::MJIBU MAOMBI**
**8.JESELY KABASA:::::::::::::::::::::::::::MJIBU MAOMBI**
**9.IMMANUEL KABASA::::::::::::::::::::MJIBU MAOMBI**
**10.EIGHTSON SICHILIM::::::::::::::::::MJIBU MAOMBI**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

Fahamu kwamba **ELIUD MBALA** amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 05/11/2024,saa 2:30 asubuhi,mbele ya Mh.T.Munzerere mwenyekiti wa Baraza.Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya. Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjini.
Kumbuka:Msipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo nyie kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 23/10/2024.

T. Munzerere
MWENYEKITI
23/10/2024

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC TANZANIA**
**IN THE SUB REGISTRY OF SHINYANGA**
**AT SHINYANGA**

**LAND APPEAL CASE REFFERENCE NO.20241016100025886**

**WILLIAM SWAI.......................................APPELLANT**

**VERSUS**

**REGINA ROBERT KISHIGA.............1ST RESPONDENT**
**SILAS M. LAZIMA...........................2ND RESPONDENT**

**TO: SILAS M. LAZIMA**

**NOTICE OF DATE OF MENTION**

**TAKE NOTICE THAT** the above appeal has been fixed for mention on the 04TH day of November, 2024. at 9:00 am Before **Hon N. L. MWAKAHESYA JUDGE.**

YOU are required to appear in this Court on the fixed date without fail. Copy of the memorandum of appeal is attached hereto and you may file your reply thereto in and serve a copy to the appellant.
**GIVEN** under my hand and the **SEAL** of the Court this 28TH day of October, 2024.

**COPY TO BE SERVED UPON** — DEPUTY REGISTRAR
**..........................................**
**Signature.........................**
**Date.................................**

## NOTISI YA TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ULIPAJI WA DENI PAMOJA NA MNADA WA HADHARA

**SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd, King Africa General Enterprises, na Rapitech Solutions Limited** kwa idhini tuliyopewa na T**ujijenge Tanzania Financial Service Ltd,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa wadaiwa na wadhamini kulipa madeni yao. Baada ya hapo hatua nyingine za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni Pamoja na uuzwaji wa mali walizoweka dhamana ya mkopo kama ilivyotangazwa gazetini.

| Mdhamini/Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Mashella Sylivester Kenemo | Gari T.107 EHN Nissan Civilian – Tabata SEPCO yard | 3/12/2024 | SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd |
| Hamida Mohamed Aley | Plot ipo Tandika-Temeke | 19/11/2024 (Marudio ya mnada) | Rapitech Solutions Limited |
| Mary Richard Mwavala / Hp Planners and Events Management | Nyumba ipo Tabata - Kisiwani | 22/11/2024 | King Africa General Enterprises |
| Omary Said Magoma/ Mwajuma Charles Magori | Nyumba ipo Mbagala - kiburugwa | 25/11/2024 | King Africa General Enterprises |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO: 0715683777/0750548337**
**King Africa :0718399636/0618989425**
**RAPITECH : 0628866132/0755264606**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie, 0677 020701***

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kamala Harris, Trump wakabana koo

**WISCONSIN,** Marekani

WAGOMBEA wa urais nchini Marekani, Kamala Harris na Donald Trump, wanazidi kukabana koo katika kipindi cha lala salama, huku kila mmoja akitumia mbinu mbadala ya kushawishi kupata kura nyingi.

Wagombea hao, Harris kutoka Chama cha Democratic na Trump wa Republican, walirushiana vijembe wakati walipojikuta wakifanya kampeni katika jimbo moja la Wisconsin hapo jana.

Zikiwa zimebaki siku sita kuelekea uchaguzi mkuu, Harris katika hotuba yake akiwa kwenye Chuo Kikuu cha Wisconsin mjini Madison, alisema ni wakati wa uongozi wa kizazi kipya kuingia madarakani nchini humo.

Mgombea huyo wa Democratic anayeongoza kwa kiasi kidogo katika kura ya maoni dhidi ya Trump, akiwa katika jimbo hilo alisema kuwa wapigakura katika uchaguzi huo wana nafasi ya kufunga ukurasa wa muongo mmoja wa Donald Trump ambaye anajaribu kuwagawanya na kuwafanya waogopane.

Aliwaeleza wafuasi wake kwamba ni wakati wa kizazi kipya kuiongoza Marekani na yuko tayari kuwapa aina hiyo ya uongozi kama raisi ajaye wa Marekani.

Harris amewaahidi wafuasi wake kuwa iwapo atachaguliwa atafanya juhudi za kutafuta suluhisho kwa matatizo yanayowakabili na kwamba hahitaji kupata alama za kisiasa bali anataka maendeleo.

Mgombea huyo alikuwa akitumia muda mwingi wa kampeni zake kuwafikia waliowahi kuwa wafuasi wa Trump na wasiokubaliana na siasa zake.

Amekuwa akiwaambia wafuasi hao wa zamani wa Trump kuwa anataka kuwashirikisha Warepublican katika Baraza lake la Mawaziri kama atachaguliwa.

**Trump na gari la takataka**

Kwa upande wake mgombea wa Republican Donald Trump, akiwa katika jimbo hilo hilo, alionekana kwenye kampeni akiwa amepanda kwenye gari la takataka hatua ambayo inatafsiriwa kuwa ni jibu kwa kauli ya Rais Joe Biden iliyotolewa hivi karibuni ilipowaita wafuasi wa Trump sawa na takataka.

Akizungumza katika mkutano huo wa kampeni katika eneo la Green Bay, Trump alifafanua kuwa, alichokisema Biden kinaakisi namna wawili hao wanavyowachukulia wafuasi wake.

Alieleza kwamba maoni ya Rais Biden ni matokeo ya moja kwa moja ya uamuzi wa mpinzani wake Harris wa kumwona yeyote asiyempigia kura kuwa ni shetani na si binadamu kamili.

Katika kampeni hiyo Trump aliongeza kuwa Biden na makamu wake wamekuwa wanaichukulia nchi nzima kuwa takataka kwa kufungua mipaka na kuruhusu mfumuko wa bei na yanayoendelea Russia na Ukraine.

Trump alisema, migogoro yote aliyoitaja isingetokea kama Marekani ingelikuwa na rais tofauti. **DW**

## Korea Kaskazini yarusha kombora hatari la ICBM

**SEOUL,** Korea Kusini

KOREA Kaskazini imerusha kombora linalodaiwa kuwa la masafa marefu (ICBM) kuelekea baharini katika pwani yake ya mashariki,

Taarifa kutoka jeshi la Korea Kusini, zilisema kombora hilo lilirushwa jana 1:10 za nchi hiyo.

Tukio hilo linakuja wakati uhusiano kati ya nchi hizo mbili jirani unazidi kuwa mbaya.

Korea Kusini ilikuwa imeonya Jumatano kwamba Korea Kaskazini ilikuwa inajiandaa kuirusha kombora lake la ICBM wakati wa uchaguzi wa urais nchini Marekani Novemba 5.

Mara ya mwisho Korea Kaskazini kurusha kombora la ICBM ilikuwa mwezi Disemba mwaka jana.

Majaribio ya makombora hayo ni kinyume na vikwazo vya muda mrefu vilivyowekwa na marekani na Umoja wa Mataifa.

Nchi jirani ya Japan ilisema kuwa ilifuatilia urushaji wa kombora hilo na kuongeza kuwa lilitarajiwa kuanguka baharini ifikapo saa 8:40 kwa majira ya nchi hiyo.

Tukio hilo la Alhamisi linakuja baada ya Korea Kusini na Marekani kuishutumu Korea Kaskazini kwa kutuma wanajeshi wake nchini Russia kusaidia vita vya nchini Ukraine.

Madai ya kuwepo kwa wanajeshi wa Korea Kaskazini nchini Russia kumeongeza wasiwasi kuhusu kuimarika kwa uhusiano kati ya Putin na kiongozi wa Korea Kaskazini Kim Jong Un. **BBC**






Mgombea urais wa Republican, Donald Trump, akiwa katika gari la takataka wakati wa kampeni yake katika Jimbo la Wisconsin nchini Marekani jana. **PICHA: ASSOCIATED PRESS**

## Israel yashambulia na kuua watu 19 Lebanon

**BEIRUT,** Lebanon



Mwonekano wa gari kubwa lililoharibiwa kufuatia jeshi la Israel kufanya shambulizi la anga kwenye barabara ya Aariya-Kahale katika Mkoa wa Mount Lebanon.

JESHI la Israel limefanya mashambulizi karibu na mji wa Baalbel nchini Lebanon na kusababisha vifo vya watu 19.

Wizara ya Afya ya nchi hiyo ilisema tukio hilo limetokea jana saa chache baada ya maelfu ya wakazi kukimbia mji huo kutokana na maagizo ya kuyahama yaliyotolewa na jeshi la Israel.

Meya wa mji huo, Mustafa al-Shell aliiambia BBC kuwa zaidi ya mashambulizi 20 ya anga yaliripotiwa kuanzia Jumatano alasiri katika eneo la Baalbek, na matano ndani ya jiji ambalo kuna jumba la hekalu la kale la Kirumi linalotambuliwa na Unesco.

Jeshi la Israel lilisema kuwa limeshambulia vituo vya kutolea amri na udhibiti vya Hezbollah na miundombinu katika mji wa Baalbek na Nabatiyeh, kusini mwa Lebanon.

Jeshi pia lilisema lililenga vituo vya mafuta vya Hezbollah katika Bonde la Bekaa, ambako mji huo upo.

Hata hivyo, halikutoa maelezo zaidi kuhusu tukio hilo.

Shirika la habari la serikali ya Lebanon lilisema matangi ya kuhifadhi mafuta ya dizeli yalipigwa mabomu katika mji wa Douris na kusababisha wingu la moshi mweusi ukipanda angani.

Mashambulizi hayo yamekuja huku katibu mkuu mpya wa Hezbollah, akisema kundi hilo litaendeleza mpango wake wa vita dhidi ya Israel chini ya uongozi wake na kwamba halitadai kusitishwa kwa mapigano.

Akizungumza siku moja baada ya uteuzi wake kutangazwa, Naim Qassem alisema atafuata ajenda ya mtangulizi wake, Hassan Nasrallah, ambaye aliuawa katika mashambulizi ya anga ya Israel mjini Beirut mwezi uliopita. **BBC**

# GEITA GOLD, MTIBWA SUGAR HAZISHIKIKI CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

GEITA Gold ya mkoani Geita na Mtibwa Sugar ya Manungu, Morogoro ambazo zilishuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliopita zimekuwa tishio katika Ligi ya Championship inayoendelea katika viwanja mbalimbali hapa nchini.

**Timu hizo zinaonekana wazi zimepania kuhakikisha zinarejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.**

Geita Gold, iko kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 14 baada ya kucheza michezo sita, ikishinda minne, sare mbili, ikifunga mabao nane na ikiruhusu nyavu zake kutikiswa mara moja.

Timu hiyo ilifanikiwa kupanda kileleni kwa mara ya kwanza tangu kuanza kwa ligi hiyo wiki hii baada ya kuifunga Mtibwa Sugar bao 1-0.

Kwa upande wa Mtibwa Sugar ambayo ilikuwa kinara wa ligi hiyo kwa raundi tano za kwanza, ilishuka hadi nafasi ya pili baada ya kupoteza mchezo huo wa ugenini.

Mtibwa Sugar imecheza michezo sita mpaka sasa, ikishinda minne, sare moja na kupoteza moja, ikikusanya pointi 13 kibindoni.

Wakati timu hizo zilizoshuka daraja msimu uliopita zikipambana huko juu, nafasi ya tatu inashikiliwa na TMA yenye pointi 12, ikicheza michezo sita, kushinda michezo mitatu na sare tatu, Stand United ikiwa kwenye nafasi ya nne na pointi 12, lakini ina mabao machache ya kufunga ukilinganisha na TMA.

Nafasi ya tano inashikiliwa na Songea United ya mkoani Ruvuma, timu ambayo ilianza ligi hiyo kwa kasi, lakini ni kama upepo umeanza kukata, ikiwa na pointi 11, Mbeya City ikiwa pia na pointi kama hizo kwenye nafasi ya sita, ikiathirika na uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa.

Mbeya Kwanza ipo katika nafasi ya saba ikiwa na pointi 10 sawa na Bigman FC zamani iliitwa Mwadui FC, ikiwa nafasi ya nane.

Timu ambazo mpaka sasa hazijafanya vizuri katika ligi hiyo ni Transit Camp ambayo ina pointi mbili tu kwa michezo sita iliyocheza ikiwa nafasi ya 14, African Sports ikiwa na pointi moja ikiwa nafasi ya 15, na Kilivya FC inaburuza mkia, ikiwa haina pointi hata moja, ikicheza michezo sita na kupoteza yote.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi za juu zitapanda moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao huku zitakazoshika nafasi ya tatu na nne zitapambana katika mechi za mtoani dhidi ya timu za Ligi Kuu.

# *Judo taifa kuchuana kesho Dar*

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Taifa ya Judo kwa mwaka huu yamepangwa kufanyika kesho kwenye Ukumbi wa DonBosco jijini Dar es Salaam imeelezwa.

Lengo la mashindano hayo ni kufanya uteuzi wa wachezaji watakayounda Timu ya Taifa ambayo itakwenda kushiriki michuano ya wazi ya Afrika itakayofanyika kuanzia Novemba 21 hadi 24, mwaka huu jijini Dakar nchini Senegal.

Akizungumza na Nipashe Katibu Mkuu wa Chama cha Judo Tanzania (JATA), Innocent Mallya, alisema yatashirikisha klabu kutoka Tanzania Bara pamoja na Zanzibar.

"Maandalizi kuelekea katika mashindano ya taifa yanaendelea vyema, kwa upande wetu kila kitu kimekamilika, tunaomba wadau mbalimbali wajitokeze ili kufanikisha jambo letu," alisema Mallya.

Aliongeza kwa sasa mchezo huo unazidi kukua tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita kwa sababu sasa watu wengi wameanza kuupenda na kuuelewa.

"Tunawakaribisha wadau kutoka sehemu mbalimbali kushuhudia vipaji ambavyo vitaonyeshwa na wachezaji wetu, hii ni nafasi nzuri ya kupandisha viwango vya nyota wetu," Mallya alisema.

Aliongeza kwa kuishukuru serikali kutokana na mchango mkubwa wanaotoa kuhakikisha Tanzania inafanya vizuri katika michezo mbalimbali.




Mchezaji wa Mashujaa FC akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuivaa Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma. **PICHA: MTANDAO**

# Tabora United vinara wa kuzawadiwa penalti Bara

**Na Adam Fungamwango**

TABORA United FC inaongoza kwa kupata penalti nyingi katika Ligi Kuu Tanzania Bara kuliko timu nyingine mpaka sasa, imefahamika.

Timu hiyo imezawadiwa penalti nne mpaka sasa katika michezo tisa iliyocheza.

Katika penalti hizo, imewekwa kwenye kamba tatu na kukosa moja.

Penalti tatu ilizipata kupitia wachezaji wake, Heritier Makambo katika mechi dhidi ya Namungo, ikishinda mabao 2-1, Shedrack Asiegbu akiifungia timu hiyo tuta pekee katika mchezo dhidi ya Kagera Sugar na Ogochukwu Morice akifunga penalti nyingine walipokutana na Pamba ikiondoka pia na ushindi wa bao 1-0.

Penalti pekee ambayo Tabora United imekosa ilikuwa dhidi ya Fountain Gate ilipopoteza kwa mabao 3-1, na straika Makambo, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ndiye aliyekosa katika mchezo huo.

Timu inayoshika nafasi ya pili kupata penalti nyingi ni Namungo ambayo imebahatika kupata penalti tatu.

Hata hivyo, timu hiyo inaonekana haina matumizi mazuri ya mikwaju hiyo, ikiwa imekosa mbili na kupata moja tu mpaka sasa.

Namungo ambayo imecheza michezo tisa, ilikosa penalti katika mchezo dhidi ya Fountain Gate ilipofungwa mabao 2-0, aliyefanya hivyo akiwa na Amza Mubarack, na Coastal Union ikishinda mabao 2-0, Djuma Shaaban akipoteza tuta hilo.

Mchezo pekee ambao ilipata penalti yake ni dhidi ya Tabora United ilipofungwa mabao 2-1, Djuma ambaye alikosa katika mchezo dhidi ya Coastal, aliukwamisha wavuni na kuipatia bao la kufutia machozi.

Hadi kufikia jana jumla ya penalti 21 ilikuwa zimepatikana kwenye Ligi Kuu, 16 zikiwekwa ndani ya nyavu na tano zikiota mbawa.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Mashujaa kuikaribisha Simba kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma wakati kesho Yanga ikikutana na Azam FC na Coastal Union itawafuata Singida Black Stars.

Mechi kati ya Fountain Gate dhidi ya Pamba Jiji sasa itachezwa Novemba 5, mwaka huu.

Mabingwa watetezi, Yanga wenye pointi 24 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Singida Black Stars yenye pointi 22 kibindoni.

## ZISIKUPITE

### AMORIM AMKATAA CASEMIRO

RUBEN Amorim tayari amezungumzia mipango yake ya uhamisho na uongozi wa Manchester United na haoni winga Antony, viungo Casemiro na Christian Eriksen au beki, Victor Lindelof kama sehemu ya mipango yake. ***(TeamTalks)***

### BARCA YAMTAKA LEAO

BARCELONA inavutiwa na winga wa AC Milan, Rafael Leao, 25, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kwa sasa akiwa hapendezwi na San Siro. ***(Sport)***

### CITY: ECHEVERRI HAONDOKI

MANCHESTER City imekataa mipango ya klabu kadhaa ya kumchukua kiungo mshambuliaji, Claudio Echeverri, 18, kwa mkopo huku raia huyo wa Argentina akitarajiwa kuungana na kikosi cha Pep Guardiola kutoka River Plate mapema mwakani. ***(Fabrizio Romano)***

### ROMA YASAKA KOCHA

AS Roma imeanza kutafuta kocha mbadala iwapo, Ivan Juric, atashindwa kushinda mechi yao ijayo dhidi ya Torino. ***(Corriere dello Sport)***

### TENA HAG ALIMTAKA WELBECK

ERIK ten Hag alifikiria kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Danny Welbeck, 33, kutoka Brighton wakati wa uongozi wake kama Kocha wa Mashetani Wekundu. ***(The Athletic)***

### LOOKMAN AGEUKA LULU

KLABU ya West Ham itakuwa na shida kuendeleza nia ya kumnunua fowadi wa Atalanta, Ademola Lookman, 27, huku Paris St-Germain ikipewa nafasi kubwa ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria iwapo atapatikana. ***(Football Insider)***

### PORRO ANUKIA MADRID

REAL Madrid itafikiria kumnunua beki wa pembeni wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya Hispania, Pedro Porro, 25, ikiwa hawataweza kukamilisha uhamisho wa mlinzi wa England na Liverpool, Trent Alexander-Arnold. ***(AS)***

### VINICIUS ATAJWA SAUDIA

KLABU za Saudi Arabia zimeonyesha nia ya kumsajili fowadi wa Brazil, Vinicius Junior, 24, kutoka Real Madrid, wakitumaini mchezaji huyo atakuwa amechoshwa na soka la Ulaya baada ya kunyimwa tuzo ya Ballon d'Or. ***(Sport)***

### MULLER AITAMANI MLS

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Thomas Muller, 35, ameonyesha nia ya kutaka kuhamia Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS), atakapoondoka Bayern Munich. ***(Bild)***

### NAPOLI YAJIPANGA ZAIDI

NAPOLI inaendelea na mazungumzo na fowadi wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, 23, kuhusu mkataba mpya, ambao utajumuisha kifungu cha kumnunua cha pauni milioni 84. ***(Sky Sports Italia)***

## DOND OKA MAGAZ AYA



# YAMAL: SASA NAITAKA TUZO YA BALLON D'OR

## ●●● Lengo lake ni kushinda tuzo hiyo mapema huku Barca pia...

**BARCELONA,** Hispania

MCHEZAJI wa maajabu wa Barcelona, Lamine Yamal, analenga kutwaa tuzo ya Ballon d'Or na anatumaini atashinda siku zijazo baada ya kutangazwa Mchezaji Chipukizi Bora zaidi duniani wakati wa sherehe zilizofanyika Jumatatu usiku.

**Winga huyo wa Hispania alitwaa tuzo ya Kopa usiku uleule ambao Rodri wa Manchester City alitwaa tuzo ya Ballon d'Or, kuashiria hadhi yake ya kuwa Mchezaji Bora wa Kiume.**

Kampeni ya mafanikio ya Yamal huko Barca ilimfanya kuwa katika kikosi cha kwanza chini ya Xavi na tayari mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 amefunga mabao sita katika mechi 14 chini ya Kocha Hansi Flick.

Mafanikio ya kijana huyo kwa klabu na nchi yamemfanya afikishe kilele cha soka duniani, na kupata nafasi yake miongoni mwa wachezaji bora zaidi.

Lakini nyota huyo ana macho yake kwenye tuzo nyingine, akifichua ndoto yake ya kushinda Ballon d'Or.

"Inashangaza kwenye tamasha hili na nataka kutafuta zaidi," alisema Yamal kupitia Movistar Plus.

"Kutafuta zaidi kunamaanisha ubingwa wa LaLiga, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Copa del Rey na kila kitu tunaweza.

"Mmoja mmoja, mwishowe wachezaji wote wana lengo la Ballon d'Or. Ninatumaini naweza kulishinda haraka iwezekanavyo, ni jambo ambalo ninalo akilini na ninalifuata."

Rodri amekuwa kiungo mkabaji wa kwanza kutwaa tuzo ya Ballon d'Or baada ya kumshinda, Vinicius Junior wa Real Madrid.

Yamal anaweza kuwa katika mstari wa kushinda tuzo ya mwaka ujao ikiwa Barca wanaweza kuendeleza kiwango chao bora cha sasa.

HABARI MICHEZO

# VAN NISTELROOY: NITABAKI UNITED




**MANCHESTER,** England

RUUD van Nistelrooy amesema yuko tayari kubakia Manchester United katika nafasi yoyote wakati kocha mpya atakapoteuliwa, baada ya kusimamia ushindi wa mabao 5-2 katika mechi ya michuano ya Kombe la Carabao dhidi ya Leicester City iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi.

Huo ulikuwa mchezo wake wa kwanza kama kocha mkuu wa muda wa United baada ya kufukuzwa, Erik ten Hag.

United wanaendelea kufanya mazungumzo na Sporting CP ili kumchukua kocha wao mkuu, Ruben Amorim, baada ya kukubali kulipa kipengele cha kutolewa cha euro milioni 10 kwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 39 ili achukue nafasi ya Ten Hag.

Lakini kwa mujibu wa ESPN, United inafanya juhudi za kuweka makubaliano na Amorim, masharti ya mkataba wake na mabingwa hao wa Ureno yanaweza kumfanya kuchelewa kuwasili Old Trafford hadi kuanza kwa mapumziko ya pili ya kimataifa Novemba 11, mwaka huu.

Ucheleweshaji kama huo wa kuwasili kwa Amorim huko United unaweza kumfanya Van Nistelrooy kubakia kama kocha kwa muda kwa mechi za Ligi Kuu dhidi ya Chelsea na Leicester City, pamoja na mechi ya Europa League dhidi ya PAOK Thessaloniki huko Old Trafford Novemba 7, mwaka huu.

Baada ya kuajiriwa na United kama kocha msaidizi wa Ten Hag majira ya joto, Van Nistelrooy alikaa miaka mitano kama mchezaji bado unaweza kuwa mfupi, lakini alisema baada ya mchezo wa Leicester atakaa muda mrefu.

"Bila shaka," alisema Van Nistelrooy akiiambia Sky Sports. "Nilikuja hapa kama msaidizi kusaidia klabu. Sasa katika jukumu hili, ninasaidia kadri inavyohitajika.

"Katika siku zijazo kwa nafasi yoyote, nitakuwa hapa kusaidia klabu zaidi kujenga kuelekea siku za usoni ndivyo niko hapa."

## Klopp atetea uamuzi wake kutua Red Bull

**DORTMUND,** Ujerumani

JURGEN Klopp ametetea uamuzi wake wa kuongoza kundi la klabu za soka zinazosimamiwa na Red Bull, akisema "sikutaka kukanyaga vidole vya mtu yoyote" baada ya uamuzi wake kuzua taharuki kutoka kwa mashabiki wa timu zake za zamani nchini Ujerumani.

Klopp anachukua nafasi ya mkuu wa kampuni hiyo ya vinywaji duniani kuanzia Januari, mwakani katika hatua iliyoonekana kuwa ya kushangaza. Itakuwa kazi yake ya kwanza baada ya kuondoka Liverpool mwishoni mwa msimu uliopita.

"Sikutaka kukanyaga vidole vya mtu yeyote, kwa hakika kabisa, na binafsi nazipenda klabu zangu zote za zamani," alisema Klopp katika mahojiano yaliyotolewa Jumatano katika podikasti iliyoandaliwa na kiungo wa zamani wa Real Madrid na Ujerumani, Toni Kroos.

Klopp alipendekeza uamuzi wowote atakaofanya kufundisha klabu nyingine pia ungewakatisha tamaa baadhi ya mashabiki.

"Kwa kweli sijui ni nini hasa ningefanya kwa kila mtu kuwa na furaha," alisema.

Red Bull, na haswa timu yake ya RB Leipzig, inachukiwa sana na mashabiki wengi wa soka wa Ujerumani, ambao wanaona uwepo wa kampuni isiyofaa inayojaribu kununua mafanikio.

Mashabiki katika klabu za zamani za Klopp kama Borussia Dortmund wamekosoa hatua hiyo, na mashabiki wa Mainz waliinua mabango mwezi huu wakionesha kusikitishwa kwao na kuhoji kama alikuwa na wazimu.

Kocha huyo wa Ujerumani alikaa Mainz kwa miaka 18 kama mchezaji na kocha kabla ya kujiunga na Dortmund mwaka wa 2008, ambapo aliiongoza klabu hiyo kutwaa mataji mawili ya Bundesliga na fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



## Arsenal yakataa kumuuza Jesus




**LONDON,** England

ARSENAL imekataa uhamisho ujao wa mshambuliaji, Gabriel Jesus, kwa mujibu wa Rais wa Palmeiras ya nchini Brazil, Leila Pereira.

Klabu hiyo ya zamani ya Mbrazil huyo imewasiliana na Washikabunduki hao kuhusu uwezekano wa kuungana tena Januari baada ya mshambuliaji huyo kutokuwa na nafasi hapo kaskazini mwa London.

Jesus ameanza mechi moja pekee ya Ligi Kuu England msimu mzima, huku Kai Havertz akiongoza safu hiyo.

Kama washindi wa Copa Libertadores mwaka, 2021, Palmeiras wanajiandaa kwa michuano ya Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia litakalofanyika mwakani nchini Marekani.

Vigogo wa Ulaya, wakiwamo Chelsea, Real Madrid na Manchester City, watakuwa katika michuano hiyo lakini Jesus hatawawakilisha waajiri wake wa zamani kwenye hafla ya kimataifa.

"Gabriel Jesus haji," alisema Pereira akiiambia ESPN.

"Tuliwasiliana na Arsenal, na wakasema, 'Leila, hakuna masharti yoyote. Hatutafanya mazungumzo na mchezaji huyo.' Mada imefungwa."

Jesus aliwaacha mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City na kujiunga na washikabunduki hao msimu wa joto wa 2022, akiwasili kama mshambuliaji chaguo la kwanza wa klabu hiyo.

Majeraha mbalimbali yameathiri misimu yake miwili iliyopita na kiwango cha juu cha Havertz kinachoendelea kuimarika katika safu ya ushambuliaji ya Arsenal kimemfanya abakie benchi.

## Gamondi: Hakuna kama Yanga

INATOKA UK. 24

mpira," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Aliongeza kupoteza mechi hiyo bado haijawafanya kukata tamaa ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

"Hatujajitoa katika njia ya kwenda kuusaka ubingwa, bado tuna matumaini makubwa ya kuwa mabingwa wa nchi hii, na kiwango cha mchezo wa leo (juzi), kimetufanya tuone kumbe inawezekana," Aussems aliongeza.

Bao la kiungo mshambuliaji raia wa Ivory Coast, Pacome Zouzoua, lililofungwa dakika ya 67, liliifanya Yanga kuendelea kupata ushindi wa asilimia 100 msimu huu.

Yanga itashuka dimbani tena kesho kuwakaribisha Azam FC wakati leo Mashujaa itawaalika Simba kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

## Simba, Mashujaa vitani Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

go vyao halisi," alisema kocha huyo.

Hata hivyo alisema katika mchezo wa leo bado atawakosa wachezaji wake wawili, ambao ni beki wa kati, Abdulrazack Hamza na Yusuph Kagoma, walioumia katika mchezo dhidi ya Yanga.

"Afadhali Hamza, anaweza kurejea mapema, ila Kagoma anaweza asionekane hata katika mchezo unaofuata dhidi ya KMC, " Fadlu alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Mashujaa, Maulid Makata, alikiri mchezo utakuwa mgumu kwa sababu wanakutana na timu kubwa lakini msimu huu ikiwa bora zaidi kuliko msimu uliopita.

Makata alisema hata hivyo wachezaji wake wanapenda kucheza mechi za aina hiyo ambazo zinawatazamaji wengi uwanjani na katika televisheni.

"Mechi kama hizi makocha kazi yetu ni kuwajenga tu kisaikolojia kwa sababu wachezaji wenyewe wanazitaka, wanajua zinaonekana na watu wengi kwa hiyo nao wanataka waonekane, wajiuze.

Tunajua wenzetu ni timu kubwa na wana maandalizi makubwa kuliko sisi, huwezi kutulinganisha na sisi, ukiangalia malengo yao ni kutwaa ubingwa na sisi kubaki Ligi Kuu au nafasi ya nne, ila katika mpira chochote kinaweza kutokea," aliongeza kocha huyo.

# AZAM YAMBAKISHA SOPU CHAMAZI HADI 2025/2026

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU ikijiandaa kuwakabili mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Azam FC umetangaza rasmi umempa mkataba mpya wa mwaka mmoja mshambuliaji wake, Abdul Suleiman 'Sopu'.

Taarifa iliyotolewa na Azam jana inasema sasa mshambuliaji huyo ataendelea kuitumikia klabu hiyo hadi mwaka 2026.

"Tunapenda kutangaza rasmi Sopu atakuwa katika klabu yetu hadi mwaka 2026, hii ni baada ya kumpa mkataba wa nyongeza wa mwaka mmoja," ilisema taarifa rasmi ya klabu hiyo.

**Sopu alisajiliwa na Azam FC mwaka juzi akitokea Coastal Union ya jijini Tanga baada ya kuonyesha kiwango bora katika msimu wa 2021/2022.**

Nyota huyo alikamilisha mazungumzo ya kujiunga na Azam siku chache baada ya kumalizika kwa Fainali ya Ngao ya Jamii iliyowakutanisha Coastal Union dhidi ya Yanga, akifunga hat-trick na kupelekea mchezo huo kwenda hatua ya matuta.

Kikosi cha Azam kilichoko chini ya Kocha Mkuu, Rachid Taoussi, kinaendelea na mazoezi ili kujiimarisha kwa ajili ya kukutana na Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 24 wakifuatiwa na Singida Black Stars yenye pointi 22 huku Simba yenye pointi 21 ikifuatia katika msimamo huo wenye timu 16.

Azam iko katika nafasi ya nne ikiwa na pointi 18 huku Kagera Sugar, Pamba Jiji na KenGold zenye pointi tano kila moja zikiburuza mkia.

Ligi hiyo inaendelea leo kwa Maafande wa Mashujaa kuwakaribisha Simba kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.




Mshambuliaji wa Azam FC, Abdul Suleiman 'Sopu' akionyesha fulana inayoonyesha ataendelea kuitumikia klabu hiyo hadi mwaka 2026 baada ya kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja jana. **PICHA: MTANDAO**

# *Fountain Gate yaiwaza Pamba*

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Fountain Gate FC kinaendelea kujinoa kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Pamba FC utakaochezwa Novemba 5, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohammed Muya, alisema malengo yake ni kupata pointi tatu katika mchezo wao huo ingawa amejiandaa kukutana na upinzani kutoka kwa wenyeji.

Mauya alisema amefanyia kazi makosa waliyobaini katika mechi iliyopita na sasa wataingia kwa tahadhari kuhakikisha wanazibakisha pointi tatu nyumbani.

"Malengo yangu ni kupata pointi tatu katika mchezo wetu huo, ingawa ninaamini utakuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa, hakuna mechi rahisi msimu huu," alisema Muya.

Aliongeza msimu huu umekuwa na ushindani zaidi kwa sababu kila timu imejipanga kuhakikisha inavuna pointi ili isishuke daraja kwa kirahisi.

"Msimu huu Ligi Kuu ina ushindani sana tofauti na msimu uliopita kwa sababu kila timu imejipanga kuhakikisha inashika nafasi ya juu katika msimamo na hakuna anayetamani kushuka daraja," alisema kocha huyo.

Naye Ofisa Habari wa timu hiyo, Issa Liponda, amesema wanawashukuru mashabiki wao kwa ushirikiano wanaowaonyesha wakati wote.

# Michezo

Ijumaa Novemba 1, 2024
Nipashe



Yamal: Sasa naitaka Ballon d'Or

UKURASA 21



Kiungo wa Yanga, Pacome Zouzoua (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Singida Black Stars, Khalid Dego, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar juzi usiku. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Mashujaa vitani Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

TAHADHARI na umakini ndio mambo muhimu yaliyoko katika akili ya Wekundu wa Msimbazi ambao wanatarajia kukutana na wenyeji Mashujaa FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

Simba inahitaji kupata ushindi wowote ili kupanda hadi nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo kutokana na kuwa na mabao mengi ya kufunga.

Simba imefunga mabao 16, ikifungwa matatu, huku Singida Black Stars ikiwa na mabao 13, zote zikiwa zimeruhusu nyavu zao kutikiswa mara tatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo na malengo yao ni kupata pointi tatu ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

Fadlu alisema anatarajia mechi hiyo itakuwa ngumu lakini wachezaji wake wamejipanga kuonyesha kiwango cha juu baada ya kupata mapumziko tofauti na walivyokuwa katika michezo iliyotangulia.

Simba ilipata mapumziko ya wachezaji wake baada ya kutocheza mchezo uliotakiwa kufanyika Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa KMC, Dar es Salaam dhidi ya JKT Tanzania, ambayo walipata ajali.

"Mchezo utakuwa mzuri, utakuwa mgumu kwa sababu Mashujaa ni timu nzuri, hata msimamo wa ligi unaonyesha hivyo, inashika nafasi ya sita, ile tumejipanga vizuri, wachezaji wangu wamepumzika vya kutosha, nadhani wengi watarudi katika viwan-

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi: Hakuna kama Yanga

**Kocha huyo ataka wapewe heshima, wasifananishwe na timu nyingine...**

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Singida Black Stars na kupanda kileleni, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kikosi chake hakitakiwi kufananishwa na timu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sababu hazifanani viwango.

Matokeo ya mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar juzi usiku yameifanya Yanga kufikisha pointi 24 na kuongoza ligi hiyo huku Singida Black Stars iliyokaa kileleni kwa muda mrefu kushuka hadi nafasi ya pili ikisalia na pointi zake 22 kibindoni.

Yanga ndio timu pekee mpaka sasa haijapoteza mechi hata moja, ikishinda michezo yake yote nane iliyocheza msimu huu.

**Gamondi alisema hayo akionekana kujibu kauli iliyotolewa na Kocha Mkuu wa Singida Black Stars, Patrick Aussems, ambaye kabla ya timu hizo kukutana alisema wamejiandaa kuikabili Yanga kama walivyojiandaa kucheza na Pamba Jiji.**

Raia huyo wa Argentina amewataka baadhi ya makocha na mashabiki wa soka nchini kuacha kuifananisha Yanga na timu nyingine kwa sababu ubora wa mabingwa hao watetezi umewaacha mbali sana.

Kocha huyo alisema huu ni wakati wa watu kuiheshimu Yanga na wasiifananishe na timu zao kwa sababu mchezo wa mpira wa miguu unamalizikia ndani ya uwanja baada ya 'maneno mengi' ya nje.

"Kuna wakati watu wawe wanaiheshimu Yanga, huwezi kutufanisha sisi na Pamba Jiji, mimi naheshimu timu zote, hata hao Pamba Jiji nawaheshimu, lakini wajue mchezo unamalizika ndani ya uwanja sio kuongeaongea nje," alisema Gamondi.

Kuhusu mchezo huo, Gamondi alisema ulikuwa mzuri na mgumu na kikosi chake kilitengeneza nafasi tano za kufunga kama wangekuwa makini, lakini akisifia kiwango bora ambacho wamekionyesha baada ya muda mrefu kupita.

"Ilikuwa ni mechi nzuri na ngumu, tulitengeneza nafasi tano za kufunga, leo (juzi), tulikuwa katika kiwango bora sana," alitamba kocha huyo baada ya ushindi huo.

Naye Aussems alikiri kufungwa kihalali, akifurahia na kujitoa kwa wachezaji wake ambao walionyesha upinzani mkali na hiyo imempa 'kiburi' bado wapo katika mbio za ubingwa msimu huu licha ya kupoteza mechi hiyo ya juzi.

"Tumeruhusu bao, lilikuwa zuri tu, katika mchezo huu tulikuwa tumejipanga vizuri, wachezaji walikuwa na muunganiko na ushirikiano, hasa kipindi cha pili.

Tulifanya inavyowezekana, lakini haikuwa rahisi kama tulivyokuwa tukifikiria, tulishambulia kutaka kupata mabao lakini tulishindwa na huo ndiyo

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002